BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,004,055,092/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 5

## KISWAHILI kuwa kwenye mitaala vyuo vya kimataifa


'Uwezo Award' tuzo inayopika wanafunzi kuwa wajasiriamali

Ukurasa 12

Nipashe TESA
Jumanne Juni 7, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Kilio taulo za kike wadau watamani 'pedi za kudumu'

Ukurasa 13

ELIMU
MARCO MADUHU, SHINYANGA

Manusura wa ndoa utotoni asherehekea kuwa darasani

• Anatamani ualimu na kuinua familia yake

MWANAFUNZI aliyenusurika kuozwa muda mfupi baada ya kumaliza darasa la saba na kufaulu kwenda sekondari, akilipiwa mahari ya ng'ombe 14, yuko shuleni baada ya juhudi binafsi za kukataa ndoa za udogoni kuzaa matunda.

Binti huyo, jina tunalo anasoma katika Sekondari ya Mwangulumbi, mkoani Shinyanga, alihitimu elimu ya msingi, nyumbani kwa mama yake anayeishi katika Kijiji cha Sayu wilayani Shinyanga.

Mtoto huyo, alilazimishwa ndoa baada ya baba yake kufanya maandalizi, akimpatia mchumba anayedaiwa alimkabidhiwa ng'ombe 14 na mali nyingine.

ALIVYONUSURIKA

Binti huyu mwenye miaka 15 alifaulu kwenda Sekondari ya Pandagichiza mkoani Shinyanga, lakini kabla ya kuingia darasani Januari mwaka huu, aliarifiwa kuwa amepata 'mume' na anatakiwa kuanza maisha mapya ya ndoa.

Anaambiwa hayo na kuonyeshwa mwenza mtarajiwa na wakwe zake waki wameshafika nyumbani kwao, lakini hakuwa tayari na hakukubali.

Alisema 'nooo' na akaazima baiskeli na kukukimbilia ofisi ya mtendaji kata wa Pandagichiza, akitembea zaidi ya kilometa 10 kuifikia na kutoa taarifa kuwa baba yake badala ya kumsomesha kidato cha kwanza, amemwandalia mume na saa chache zijazo anamuoza.

Wasichana na wavulana wana haki ya kusoma, waendelezwe kielimu badala ya kuozwa udogoni. PICHA: MTANDAO

Ofisi ya Mtendaji ilitoa taarifa dawati la polisi ili kumkamata mtuhumiwa, lakini alitoroka kabla ya kutiwa pingu, ikiwa ndiko kuokoka kwake.

Ndizo athari za mila na desturi kandamizi mkoani Shinyanga, zisizowathamini watoto wa kike, kuwageuza vitega uchumi vya familia na kuwabagua katika elimu na pale wanapohitimu darasa la saba au wakipevuka, hutafutiwa waume na kuwaozwa ili familia zinufaike kwa mali au mifugo.

Nipashe ilipata taarifa za tukio la mwanafunzi huyo kuozwa na baba yake na kuzichapisha Machi 1 2022, makala ikiwa na kichwa cha habari "Baba kuuza mabinti wakimaliza la saba, anawaandalia wachumba".

Habari hiyo ilichangia kumnusuru na ndoa ya utotoni, ikiwaamsha wadau mbalimbali na viongozi wa serikali kutoa maagizo ya kufuatiliwa wanafunzi wote ambao wamehitimu darasa la saba na kufaulu wafuatiliwe na ambao wameshaozeshwa waondolewe kwenye ndoa na wapelekwe shule.

John Myola ni Mkurugenzi wa Shirika la Agape ambalo linalea wasichana walioathirika na matukio ya mimba na ndoa za utotoni, anasema baada ya kupata taarifa ya mwanafunzi huyo kutaka kuozeshwa, walimsaidia na kumsomesha katika shule ya Sekondari ya Mwangulumbi iliyoko Chibe Manispaa ya Shinyanga.

Anasema shirika hilo limekuwa likiwasomesha watoto hao walioathirika na mimba na ndoa za utotoni tangu mwaka 2015 mpaka sasa na kwamba wameshasomesha wanafunzi 267, tisa wamehitimu vyuo vikuu, 22 bado wanaendelea na vyuo, wengine wakisoma kidato cha sita, tano na sekondari.

SHULE RAHA

Akizungumza na Nipashe iliyomtembelewa shuleni, binti huyo, anaeleza kufarijika sana kuwa darasani kidato cha kwanza na anaamini atatimiza ndoto zake za kuwa mwalimu na msaada kwa familia yake na waathirika wengine.

Anakumbushia kuwa siku alipotaka kuozwa na baba yake mzazi, alijisikia vibaya akikumbuka namna dada zake walivyoozwa wakiwa watoto, mateso na masumbuko wanayopitia, ugumu wa maisha na machozi kila wakati, ndipo alipogoma ili kwenda shule licha ya baba yake kung'ang'ania aolewe sababu alishachukua mahari ya ng'ombe 14.

"Baba yetu haishi nasi amem-

INAENDELEA UK.14

# Nipashe

Jumanne Juni 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580969
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Samia aagiza umakini miradi mipya ya maji ya trilioni 1.7/-

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akishuhudia utiaji saini mikataba ya miradi ya maji kwa ajili ya miji 28 kwa makandarasi walioshinda zabuni, katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## DC ataka mwalimu mtuhumiwa ubakaji wanafunzi kukamatwa

UKURASA 7

## Arusha kinara matukio ya ukatili kwa watoto

UKURASA 4

MICHEZO SIMBA, YANGA ZADAIWA BIL. 10/- UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

# Chanzo ajali iliyoua wanafunzi UDOM chatajwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limetaja chanzo cha ajali iliyosababisha vifo vya watu wanne wakiwamo wanafunzi watatu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), kuwa ni mwendo kasi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Martine Otieno, alisema mwendo kasi wa gari aina ya Toyota RAV4 yenye namba T 857 DNE lililokuwa likiendeshwa na Asanterabi Ntundu ilihama njia na kwenda upande wa pili ilipokuwa bajaji yenye namba MC 517, kugongana uso kwa uso.

Aliwataja waliofariki kuwa ni Mpeli Mahenge, Hana Zilampenda, Fortunate Kingazi na dereva wa bajaji Peter Peter.

Kamanda Otieno aliwataja majeruhi kuwa ni Agnes William abiria wa gari la RAV4 na wanafunzi ambao ni, Enika William, Asela Mey, Fide Julius, Sifa Shola na Furahini Fute.

Kamanda Otieno alisema bajaji hiyo iliwabeba wanafunzi nane, huku dereva akiwa wa tisa, kitendo ambacho kinavunja sheria ya usalama barabarani kwani kwa uhalisia bajaji inabeba abiria watatu.

Hivyo, Kamanda Otieno aliwataka raia pamoja na wanafunzi kuacha tabia ya kupanda idadi kubwa kwenye vyombo vya moto.

"Nawaomba raia muwe makini na usafiri mnaoutumia msilazimishe kupanda wengi ili hali wanatakiwa kupanda idadi ndogo ya watu,"alisema Kamanda Otione.

Alisema madereva pindi wanapokuwa barabarani wanapaswa kuwa makini na uendeshaji wao kwa kuzingatia mwendo kasi ambao ndiyo huwa chanzo cha ajali mara kwa mara.

**MIILI YAAGWA**

Akizungumza kwenye ibada ya kuaga miili ya wanafunzi hao, Mkuu wa Ndaki ya Elimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Prof. Julius Nyahonga, alisema menejimenti ya chuo watakaa ili kuomba barabara zinazopita maeneo ya chuo ziwekewe matuta.

Prof. Nyahonga pia aliwataka wanafunzi wa chuoni hapo kuacha kutumia zaidi usafiri wa bajaji na pikipiki pindi wanapokuwa na safari za kwenda mjini, badala yake watumie daladala ambazo ni uhakika kwa usalama upo.

"Mjue kuna wanafunzi 32,000 chuoni, hapa kwenye kitivo hiki wapo karibu 9,000, hatuna sababu ya kuwalaumu wanafunzi kwa sababu walitoka kwenye mambo ya dini na haikuwa usiku," alisema Prof. Nyahonga.

Aliongeza: "Umri mlionao kwenda mjini usiku na bodaboda na bajaji punguzeni na mkienda mrudi mapema kwa daladala, angalau zina nafuu. Inatuumiza sana maumivu tunayopata wazazi wenu ni makubwa, sisi ni walimu wenu lakini ni wazazi pia."

Mchungaji Emanuel Mabula aliyeongoza ibada ya kuwaaga miili ya wanafunzi hao, alisema: "Hatuwezi kulaumu kwa sababu kazi ya Mungu haina makosa."

Alisema mwanadamu yoyote lazima ataonja umauti, kwamba kifo kipo muda wowote, hivyo wanapaswa kuomba na kuwaombea wenzao waliotangulia.

**MAJERUHI WAELEZA**

Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo, Mkazi wa Ng'ong'ona, jijini hapo, Fide Julius, alisema alialikwa kwenye mahafali ya ndugu zake wanacasfetha Tayomi katika Kitivo cha Sayansi ya Jamii UDOM.

Alisema: "Nilifika kwa kuchelewa lakini nilikutana na ndugu zangu ambao ni wadogo zangu niliwaacha mwaka wa pili tukaongea, tukafurahi, tukacheka hadi muda wa kula na kukata keki, ilipofika mida ya saa 12 jioni kwasababu sherehe iliwahi kuisha tukaanza taratibu za kurudi nyumbani.

"Mimi nilikuwapo UDOM mwaka 2018 hadi 2021 nilihitimu na nikabaki hapa hapa Dodoma kwa hiyo baada ya kupata usafiri wa bajaji tulipanda watu nane kwenye ile bajaji kama ninavyokumbuka, nyuma tulikaa watu sita tuliobebana na mbele walikaa watu wawili." Alisema na kuongeza:

"Tulianza safari ya kurudi, nakumbuka nilisikia sauti ya mtu huwa namuita Mama Fortunate Kingazi alianza kusema jamani mbona hilo gari linatufuata kwa mbele, baadaye gari ikapita ndiyo sikukumbuka kilichoendelea nimejikuta nimefikishwa mahali hapa,"alisema.

Mwanafunzi Mpeli, Hana na Fortunate walikuwa wanafunzi wa Shahada ya Ualimu katika Sayansi mwaka wa tatu.

Mwili wa Mpeli umesafirishwa kwenda Mbeya, mwili wa Fortunate umesafirishwa kwenda Morogoro na Hana kwenda Kigoma kwa ajili ya taratibu za mazishi.




Majeneza yenye miili ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) waliofariki kwa ajali, yakiwa nje ya jengo la mochwari ya Hopitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma jana, wakati ya ibada ya kuaga na kusafirishwa kuelekea mkoani Kigoma, Mbeya na Morogoro, kwa ajili ya mazishi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Samia aagiza umakini miradi mipya ya maji ya trilioni 1.7/-

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaagiza wahandisi wa Wizara ya Maji kusimamia makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji yenye thamani ya shilingi trilioni 1.7 katika miji 28, wawe makini wasiitie serikali hasara kwa kutoikamilisha. Alitamka hayo jijini Dodoma katika tukio la utiaji saini mikataba ya miradi ya maji kwa miji 28 ya Tanzania Bara, sambamba na upelekaji wa fedha za miradi hiyo Zanzibar.

Rais alitoa angalizo fedha hizo zitumike vizuri, kwa kuwa ni mkopo utakaolipwa na Watanzania wote, hivyo ni muhimu usimamiwe, ili watakapolipa uwe wasaa unaoendana na manufaa yake wakati huo.

"Wahandisi wa wizara kasimamieni makandarasi, kila mfanyabiashara lengo lake ni 'ku-maximize profit' (kuongeza faida), sasa mwingine anaamua 'ku-maximaize profit' akakutia wewe hasara.

"Nendeni kawasimamieni, tuhakikishe miundombinu inajengwa ipasavyo, maji yanapatikana, mkandarasi apate na sisi tupate," alifafanua, kuhusu mradi ambao thamani yake halisi ni dola za Marekani milioni 500.

Aidha, Rais Sania alipongeza Wizara ya Maji kwa kubana matumizi katika utekelezaji miradi yake, hali inayowezesha kufika maeneo mengi, katika kukidhi matarajio yao.

"Hata katika mradi huu ambao mnatekeleza sasa hivi, mmejitahidi kubana matumizi, mradi mmoja unazaa fedha za kuanzia mradi mwingine," alisema Rais Samia, akitaka iwe katika namna endelevu.

Alisema lengo la serikali lililopo kitaifa ni kuhudumia majisafi na salama kufikie asilimia 85 vijijini, huku akiishukuru serikali ya India, kwa kuwa mshirika mkubwa wa utekelezaji miradi ya maji nchini.

Mkuu huyo wa nchi alitaja baadhi ya vyanzo kuwa ni mradi wa Ziwa Victoria, ambayo kupitia Benki ya Exim nchi hiyo iliipatia serikali Sh. bilioni 617 iliyosaidia kusambaza maji katika maeneo ya Tabora, Igunga na Nzega ikinufaisha vijiji 102.

"Mradi huu tunasaini ni matokeo ya ushirikiano mzuri baina ya serikali yetu na serikali ya India ambapo imeweza kuipatia Tanzania mkopo wa dola milioni 500," alisema.

Kuhusu miradi ya maji iliyoko Same na Mwanga mkoani Kilimanjaro, utekelezaji wake umechukua muda mrefu, Rais Samia, alisema utekelezaji wake unaendelea na unahitaji Sh. bilioni 36 kukamilika, akiahidi kutafuta pesa za kuukamilisha mwakani.

Kwa mradi wa Dodoma aliahidi kushauriana na wataalamu wa nishati, kuiona namna ya kuwezesha kutumia maji ya Bwawa la Mtera kusambaza maji katika jiji hilo.

"Tunafikiria tuchukue maji Mtera tusambaze Dodoma angalau kwa asilimia moja. Wenzetu wa nishati tutakaa tuzungumze kwa pamoja," alisema.

Naye Waziri wa Maji, Juma Aweso, alimhakikishia Rais Samia kuwa wataisimamia miradi hiyo ikamilike kama inavyotarajiwa, ili kuwanusuru watumiaji na hasa kinamama na athari zinazotokana na uhaba wa maji.

"Ssisi viongozi wa Wizara ya Maji tutafia 'site' (eneo la kazi), hatutocheka na mkandarasi, hatutocheka na mtaalamu ambaye tunaona kabisa huyu anatukwamisha katika utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi," aliahidi Waziri Aweso.

Aliitaja baadhi ya miji itakayonufaika katika mradi huo kuwa ni Handeni, Korogwe, Pangani, Kilwa Masoko, Nanyumbu, Ifakara, Chunya, Rujewa, Wanging'ombe, Makambako, Njombe, Kiomboi, Singida, Manyoni, Chemba na Chamwino.

Mingine kwa Mujibu wa Waziri Aweso ni; Kasulu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Kayanga, Geita, Chato, Mafinga, Newala, Tandahimba, Nanyamba, Rorya na Songea.

Alisema, ndani ya mwaka mmoja sasa miradi ya maji katika wizara hiyo imetekelezwa kwa asilimia 90, huku bajeti ya maji kwa mwaka huu wa fedha tayari imeshapitishwa.

Alisema kupitia Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), watatekeleza miradi ya maji 1029 katika mwaka uliopo wa fedha, kupitia gawiwo la fedha za UVIKO la Sh. bilioni 132 itakayojenga miradi 232 ya maji katika kila jimbo, ikiwamo kununua mitambo ya kuchimba visima.

## Migogoro Wilaya Chemba yamchefua waziri Bashungwa

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amekerwa na migogoro ya mara kwa mara wilayani Chemba ambayo inasababisha watumishi wengi kuomba uhamisho.

Akiwa wilayani humo, Bashungwa alisema hafurahishwi na migogoro inayoendelea katika wilaya hiyo na kuwataka wahusika kuchukua hatua kuimaliza.

"Nimekuja hapa Chemba na kuwakumbusha hebu tukae kabla mambo hayajaharibika. Kwanza hapa Chemba mnapata sifa ya kuwa na migogoro kila siku na kama mnavyofahamu kwenye migogoro maendeleo hayawezi kufanyika kwa weledi," alisema Bashungwa na kuongeza:

"Hili la migogoro si jambo jema, nimekuja kuwasikiliza kwani mnagombana, mnavutana, mnajua mivutano hii inakwamisha utekelezaji wa ilani ya CCM? Sipo tayari kumwangusha Rais Samia katika kutekeleza ilani, kama kuna mtu mwenye nia hiyo basi niondoke nikijua madiwani hawako tayari kuwa na sisi kutekeleza," alisema. Bashungwa alisema sababu ya pili ni kuwapo wimbi kubwa la watumishi wa Halmashauri ya Chemba kuomba uhamisho.

"Jambo la pili ni wimbi la watumishi kuhama kutoka Chemba linaongezeka. Sasa Mwenyekiti wa Chama, Mkurugenzi, Mkuu wa wilaya mtaweza kufanya kazi bila kuwa na watumishi? Ningekuwa natoa vibali kutokana na kasi ya watumishi wanavyotaka kuhama mtabaki viongozi peke yenu, mheshimiwa utaweza kufundisha hapa shuleni kama walimu wataondoka? Mheshimwa Mkuu wa Wilaya unajua kushika chaki? Naamini tutakaa kama watu wazima kujua tatizo nini, kama tutaruhusu uhamisho hakuna mtumishi atakayebaki katika Wilaya ya Chemba. Sasa kuna siafu? Au kuna nini kinawafanya watumishi wasiwe na amani," alihoji.

Katika kikao hicho walijadili pia, mwenendo wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani humo na kutoa maelekezo.

"Kamati ya siasa ni chambo kikubwa, ndicho kinasimamia serikali kwa maana ya halmashauri, serikali ya wilaya, kumekuwa na matatizo ambayo baada ya kukaa tumeona hakuna haja ya kuwa na kikao kingine hapa," alisema Bashungwa.

Alisema lengo la hatua hiyo ni kujenga Halmashauri ya Chemba yenye umoja na mshikamano.

"Tunataka kujenga Halmashauri ya Chemba yenye umoja na mshikamano katika kutekeleza ilani ya CCM, wataalamu wakiwa kaskazini na baraza likiwa kusini mtakutana wapi kujadili vipaumbele vya maendeleo, kwa hiyo tumegundua jambo hilo ndiyo tatizo kubwa ndani ya Chemba."

"Sisi serikali inayosimamiwa na CCM hatutaruhusu hiyo hali. Kwa hiyo kwenye kikao cha ndani tumekubaliana namna ya kuisimamia hii halmashauri na kujenga umoja na mshikamano."

# Mchakato wa kuandaa sheria inayokidhi mazingira mbioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira imeanza mchakato wa kuandaa Sheria ya Mazingira ambayo itakidhi matakwa ya Sera Mpya ya Mazingira ya mwaka 2021.

Waziri wa Ofisi hiyo, Dk. Selemani Jafo alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na maofisa mazingira wa mikoa na wilaya nchini. Dk. Jafo aliwaagiza maofisa mazingira kote nchini kuitafsiri na kusimamia utekelezaji wa sera hiyo.

Aidha, alisema takwimu zilizoko duniani zinaonyesha kila mwaka asilimia moja ya pato la taifa hutumika kushughulikia kero za kimazingira na ifikapo mwaka 2030 itakuwa ni asilimia tano, kuna kila sababu ya kusimamia kwa ajenda ya mazingira.

"Asilimia 65 wanategemea kilimo na asilimia 27 ya pato la taifa linachangiwa na sekta ya kilimo, huku asilimia 29.2 ya mauzo ya nje yanategemea kilimo, hii ina maana mazingira yanapoathirika na uchumi unaathirika," alisema Dk. Jafo.

Alisema mikoa na halmashauri nyingi hazijatoa kipaumbele kikubwa kwenye usafi na usimamizi wa mazingira, jambo ambalo linafanya maeneo mengi kuwapo na uchafu, na kuwataka wataalamu hao kwenda kusimamia suala hilo.

Waziri Jafo alisema lengo la serikali ni kupata miti milioni 276 kila mwaka ikiwa kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 na kuwasisitiza wataalamu hao kusimamia suala hilo, ajenda ya upandaji miti iwe endelevu na ifanye vizuri.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye matumizi makubwa ya nishati ya kuni na mkaa jambo ambalo linafanya kupoteza takribani hekta laki nne kila mwaka na kusisitiza lazima kasi ya upandaji miti iongezeke. Waziri Jafo alisema serikali imehakikisha asilimia 32.5 ya ardhi yake imehifadhiwa, miti hekta milioni 48.1 imehifadhi sambamba na kuendesha kampeni mbalimbali za mazingira na kuhimiza maofisa mazingira kutunza uhifadhi huo na kusimamia kikamilifu kampeni hizo.

Aidha, aliagiza Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuhakikisha inaanzisha vitalu vya miti katika shule hali ambao inapunguza utegemezi wa miti na kuongeza kasi ya upandaji wa miti.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alipofika Ikulu, jijini Zanzibar jana, kwa mazungumzo na kumuaga kufuatia kumaliza muda wa utumishi wake ndani ya jeshi hilo mwishoni mwa mwezi huu. **Habari Uk. 17.** **PICHA: IKULU**

## Ahukumiwa mwaka 1 kifungo cha nje kujaribu kuua bila kukusudia

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Jaji wa Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu Maziku Faida (52), kutumikia kifungo cha nje mwaka mmoja kwa kosa la kujaribu kuua kwa kumchoma mtu kisu tumboni hadi utumbo kutoka nje.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Jaji wa Mahakama hiyo, Liliani Itemba, baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa lake.

Awali, Jaji Itemba alimwambia Wakili wa Serikali, Janeth Kisibo, kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Wakili Kisibo alidai kuwa Septemba 19, 2016 mshtakiwa akiwa na mlalamikaji, Majuto Bangaya, wakinywa pombe, mlalamikaji alimkuta mshtakiwa akiwa amekalia kiti chake na alipomwomba atoke alikataa kitendo kilichosababisha waanze kupigana na mshtakiwa alipozidiwa nguvu alichukua kisu na kumchoma mlalamikaji tumboni.

Wakili alidai tukio hilo lilisababisha wasamaria wema wamsaidie majeruhi kumpeleka Kituo cha Polisi Geita na kupewa fomu ya PF3 kwa ajili ya kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya Geita.

Alidai pia, mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi na baada ya mahojiano alifikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabili.

Baada ya kusomewa maelezo hayo, Jaji Lilian alimuuliza mshtakiwa kama maelezo hayo yana ukweli, ndipo alipojibu kuwa ni kweli.

Kitendo cha mshtakiwa kukiri kosa, Jaji Lilian alisema mahakama inamtia hatiani kwa kosa la kujaribu kuua bila ya kukusudia.

Mshtakiwa huyo aliyekuwa akitetewa na Wakili wa kujitegemea Nestory Kuyula, aliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa sababu ni kosa lake la kwanza pia ana familia pamoja na ndugu wanaomtegemea.

Jaji Lilian alitupilia mbali utetezi huo kumhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha nje cha mwaka mmoja huku akitakiwa kutotenda kosa lolote ndani ya mwaka mmoja.

Aidha, alisema kama kuna upande wowote ambao haujaridhika na hukumu hiyo, rufani ipo wazi.

Akisoma hati ya mashtaka jana Msaidizi wa Kumbukumbu wa Mahakama Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza, Josephine Mhina, alidai kuwa Septemba 19, 2016 majira ya saa mbili usiku eneo la Mkoani, Kata ya Kalangalala mkoani Geita, mshtakiwa alijaribu kumuua Majuto Bangaya kwa kumchoma kisu tumboni na utumbo kutoka nje.

# 'Coco Beach' kuwa eneo la uwekezaji

**Na Mary Geofrey**

MANISPAA ya Kinondoni imesema imejipanga kuhakikisha eneo la 'Coco Beach' linakuwa la uwekezaji, kivutio na utunzaji wa mazingira.

Ofisa Elimu Manispaa hiyo, Theresia Kyara, alieleza mikakati hiyo jana mkoani Dar es Salaam, wakati wa upandaji wa miti uliofanywa na kampuni binafsi ya mipango miji na wauzaji wa viwanja Property Ltd kwa lengo la kuboresha mazingira hayo.

"Manispaa tumejipanga ipasavyo kufanya mabadiliko eneo la ufukwe wa Coco Beach na tayari wawekezaji wamejitokeza kuanza biashara, mtu ambaye hajafika Coco muda mrefu aje aone kulivyokuwa na kunavyopendeza," alisema.

Alisisitiza kuwa, mbali na miti inayopandwa na kampuni ya Property eneo lote la fukwe na utengenezaji wa bustani nzuri za maua, ujenzi wa vibanda vinavyovutia, watu watapumzika na familia zao au faragha.

Alisema lengo ni kuhakikisha kunakuwa na uboreshaji wa mazingira, kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan alivyoelekeza akitaka kuona Coco Beach inakuwa kivutio na kuondokana na mazingira machafu yasiyopendeza katika maeneo hayo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya Property, Haleem Zahran, alitoa wito kwa wadau wa ardhi, zikiwamo kampuni binafsi na serikali kuhakikisha wanaweka viwango maalumu vya uuzaji ardhi ili kupata eneo la kupanda miti na kusimamia mipango miji.

Alisema, mpango wa kupanda miti Coco ni mwendelezo wa kampuni hiyo kuunga mkono jitihada za Rais Samia katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi na utunzaji wa mazingira.

"Kwetu ukinunua kiwanja kinakuwa kimepimwa, kina hati na kipo katika mipango miji na lazima kuna eneo limetengwa kwa ajili ya huduma za kijamii na katika kila eneo la ujenzi kuna mita zimetolewa za kupanda miti," alisema

# Arusha yatajwa kinara ukatili watoto

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ametaja mikoa mitano kinara kwa matukio ya ukatili wa watoto kwa mwaka 2021, huku Mkoa wa Arusha ukiongoza kuwa na idadi kubwa ya matukio hayo.

Amesema kati ya matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa katika Jeshi la Polisi ni 11,499, makosa yaliyoongoza kwa idadi kubwa ni ubakaji (5,899), mimba kwa wanafunzi (1,677) na ulawiti (1,114).

Waziri Gwajima aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa tamko kuhusu maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2022 katika Shule ya Msingi Mnadani, kuwa kwa mwaka huu itaadhimishwa kila mkoa.

Alisema mikoa iliyoongoza kwa kipindi hicho ni Arusha (808), Tanga (691), Shinyanga (505), Mwanza (500) na Mkoa wa Kipolisi Ilala (489).

"Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2021, jumla ya matukio ya ukatili kwa watoto yaliyoripotiwa katika Jeshi la Polisi ni 11,499 ikilinganishwa na matukio 15,870 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Huu ni upungufu wa matukio 4,371 sawa na asilimia 27.5,"alisema.

Waziri Gwajima alisema pamoja na jitihada mbalimbali za kutoa elimu kuhusu ukatili na madhara yake, bado kuna ongezeko la taarifa za vitendo vya ukatili wa aina mbalimbali ikiwamo ubakaji, ulawiti, utumikishwaji wa watoto katika ajira hatarishi, ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni.

"Kuna uwezekano mkubwa kwamba matukio ya ukatili yanaweza kuwa mengi kuliko haya ukizingatia kwamba haya ni yale tu yaliyotolewa taarifa kwenye vituo vya polisi.

"Taarifa zinaonyesha asilimia 60 ya ukatili unafanyika majumbani mbele ya familia zenu, tunaona baadhi ya watoto wanakatiliwa na baba zao, wajomba zao, jana nimesikia mkoa fulani kuna bibi kazi yake ni kumfinya mtoto tena kwa kisu hadi kumtoa nyama," alisema.

Kuhusu tukio la bibi kumfinya mjukuu, Waziri Gwajima alisema alituma watu kufuatilia tukio hilo na wameshamkamata mhusika na kufikishwa polisi.

"Watoto mnapokatiliwa mseme msiogope, mwambie mtu unayemuamini kama ni mwalimu ama baba au mama, kama amekukatili baba mwambie mama, mwambie jirani mwambie mtu unayemuamini.

"Pia, takwimu zinaonyesha asilimia 40 ya ukatili unatokea shuleni kuna walimu wanakatili watoto, wanawapa adhabu zilizokithiri, wengine wanabaka na kulawiti watoto na baadhi ya watoto wameanza tabia mbaya wanawalawiti na kuwabaka na kulindana,"alisema.

Aliwataka watoto kufunguka na kutokubali kukatiliwa na kwa usalama wao wajiepushe kwenda kwenye maeneo ambayo ni hatari na kuwa karibu na watu wasiowafahamu au wanaotaka kuzoea miili yao.

"Mzazi mruhusu mtoto ashiriki mabaraza na klabu za watoto shuleni kwa kuwa inajenga uwezo wa mtoto katika kufikiri, kujiamini na kujieleza, hakikisha mtoto hatumii vifaa vya kielektroniki kama simu na runinga bila uangalizi wa karibu ili kumwepusha kufanyiwa ukatili wa mtandaoni," alisema Waziri Gwajima.

Vile vile, Waziri Gwajima aliwahimiza wazazi kuzungumza na watoto wao na kufuatilia mienendo kila mara ili kuwaepusha na vitendo vya ukatili ikiwa pamoja na ubakaji, ulawiti na mimba.

Pia, aliwataka Maofisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii katika mikoa na halmashauri kuimarisha utoaji wa elimu ya malezi na makuzi ya watoto kwa wazazi na walezi.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwaasa wazazi na walezi kutambua kwamba ulezi wa sasa ni tofauti na zamani, wazungumze na watoto wao ili kujua vikwazo vinavyowakabili.

Pia, aliwataka wazazi kuwa makini na wageni wanaowakaribisha kwenye nyumba zao na kuwaruhusu kulala na watoto.



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Profesa Florens Luoga (katikati), akisalimiana na Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Afrika, Nehemiah Kyando Mchechu, alipofanya ziara ya kikazi kwenye ofisi za benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Afrika, Adam Mihayo na (wapili kushoto) ni aliyekuwa Naibu Gavana, Dk. Benard Kibesse. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkumbo ataka marekebisho baa kufanya biashara mchana

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

MBUNGE wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, ameitaka serikali kupitia upya sheria inayozuia watu kufurahi muda wote ikiwamo kunywa pombe, pamoja na kuruhusiwa kufanya biashara usiku na mchana.

Akichangia mjadala wa makadirio ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Profesa Mkumbo, alisema juzi alikutana na daktari mmoja anayefanyakazi moja ya hospitali za serikali anayeishi Kata ya Makuburi, akimlalamikia kuwa kila siku mara tatu kwa wiki anakamatwa akinywa bia asubuhi.

Alisema anafanyakazi chumba cha kuhifadhia maiti usiku, anatoka asubuhi, kabla hajaenda nyumbani hunywa bia sita na kila akienda anakamatwa. "Nikakutana na wafanyabiashara wakalalamika hawaruhusiwi kufungua baa asubuhi mwisho saa sita usiku, nikajiuliza tatizo ni nini," alihoji na kuongeza:

"Niligundua kifungu cha 14 cha sheria kinapangia watu muda wa kufurahi ni kuanzia saa sita mchana na mwisho wa kufurahi saa sita usiku. Majiji yote duniani hufanyakazi saa 24, hii habari watu wasifungue biashara, baa na wasifurahi hadi saa sita mchana ni sheria ya kizamani."

Profesa Mkumbo alisema sheria hiyo ilitungwa mwaka 1968, mwaka mmoja baada ya Azimio la Arusha, wakati nchi ikiwa ni ya wakulima na wafanyakazi na ilikuwa na lengo la watu wakafanye kazi shambani na ofisini, lakini kwa sasa ni nchi ya wafanyabiashara, wana burudani na michezo.

"Kisaikolojia maisha ni nini? Ni mchakato wa kutafuta furaha, jambo lolote linaleta furaha ni muhimu likaungwa mkono, moja ya kazi ya msingi ya wizara hii ni furaha," alisema na kuongeza:

"Hii sheria inazuia furaha ya nchi, tuiangalie tuibadilishe ili watu wawe na uhuru wa kufurahi wakati wote," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima, aliomba mwongozo alisema: "Furaha haiko ya aina moja, ziko aina nyingi, kama hawawezi kuipata furaha inayotokana na kunywa pombe basi wapate furaha inayotokana na vitu vingine."

Akijibu hoja hiyo, Prof. Mkumbo alisema haipokei taarifa hiyo na kwamba "kabla hajaziponya (Askofu Gwajima) hizo roho lazima tuponye miili ili upate roho."

Kwa mujibu wa Prof. Mkumbo, Dar es Salaam, ni Jiji la biashara na haiwezekani kupanga muda wa kufanya biashara.

"Amueni moja, Dar es Salaam watu wanafanyakazi saa 24, mtu anafanya kazi usiku ana haki ya kwenda kufanya burudani asubuhi, tuangalie sheria hii tuibadilishe tufanye biashara muda wote serikali ikusanye kodi.

## Shaka aagiza m'biashara 'tapeli' wa pembejeo kukamatwa

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kumkamata na kumchukukulia hatua mfanyabiashara wa pembejeo anayetumia vibaya majina ya viongozi akiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ili kujinufaisha katika biashara yake ya pembejeo feki za kilimo.

Shaka aliyasema hayo wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara yake ya kikazi mkoani Mtwara, akisema kuwa mfanyabiashara huyo anauza pembejeo zisizokidhi viwango huku akidai ni mali ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

"Niviombe sana vyombo vya ulinzi na usalama vitusaidie katika jambo hilo. Lakini kwa masikitiko makubwa yupo mfanyabiashara ni dalalali wa pembejeo, na yeye tayari ana pembejeo na kwa taarifa ni pembejeo feki. Anawashawishi wananchi kwamba pembejeo za serikali zimechelewa tutawauzia kwa bei hafifu.

"Bahati mbaya sana mfanyabiashara huyo anatumia jina la Waziri Mkuu kwamba hiyo ni mali yake na yeye amepewa uwakala. Vyombo vya ulinzi na usalama huyo mtu bado yupo tu mtaani kweli sijui kwa sababu ana nguvu ya fedha sijui kwa kweli na bahati nzuri nilipopata taarifa na nikapata ushahidi nilimtafuta Waziri Mkuu, nikamwambia."

Alisema Waziri Mkuu amemjulisha hajawahi kufanya biashara ya pembejeo si Mtwara, sio sehemu yoyote hausiki na hilo jambo na ameshangaa vyombo vya ulinzi na usalama havijamkamata.

Shaka alivitaka vyombo vya ulinzi kumkamata mtu huyo na kumchukulia hatua stahili huku akiamini hata mawakala wake wakitiwa nguvuni watatoa ushirikiano kwa kuonyesha yaliko maghala wanakohifadhia pembejeo hizo zisizokidhi viwango vya ubora.

"Cha kusikitisha na kustaajabisha hata hao madalali wake wanakamatwa, wanawekwa ndani baada ya muda wanatoka nje. Kwa bahati mbaya sana wengine madiwani wetu wanahusika katika huo mchezo halafu mnatupigia simu fulani kakamatwa, akamatwe tu aende huko kwa sababu hauwezi kuhujumu na sisi tukuunge mkono," alisema.

Akisisitiza alisema CCM haiwezi kukubali kuona hujuma kama hizo zinaendelea kufanyika, itaendelea kuisimamia serikali kuhakikisha wakulima wa korosho wanufaika.

Aliwataka viongozi na watumishi wa chama na serikali kuhakikisha wanafanyakazi kwa uadilifu ili kutatua changamoto zinazowakabili.

Katika mkoa wa Mtwara, alisema changamoto kubwa ni maji na baadhi ya wilaya hali ni mbaya kwa kuwa yanapatikana kwa asilimia 15 na kutoa mfano wa Wilaya ya Tandahimba.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuwapo juhudi kubwa za serikali za kuleta fedha kumaliza changamoto hiyo, jambo la kusikitisha kumekosekana usimamizi mzuri kwa miradi mingi kiasi cha kutekelezwa chini ya kiwango, kuchukua muda mrefu kukamilika na baadhi kutotoa maji.

Alizitaka mamlaka husika kuendelea kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili wananchi wapate majisafi na salama kwa uhakika.

# Vyuo vikuu nje vyaanza kufundisha Kiswahili

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

VYUO vikuu vya Ethiopia, Msumbiji na Nigeria, vimeingiza kwenye programu zao lugha ya Kiswahili kama somo rasmi litakalofundishwa kwa wanafunzi kwa lengo la kukuza lugha hiyo.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake.

Alisema kutokana na nafasi ya Kiswahili kwa sasa, lugha hiyo inaendelea kushamiri na kuvifanya vyuo vikuu vya nje ambavyo awali havikuwa na programu za Kiswahili kuanza harakati za kuingiza lugha hiyo.

"Tayari kuna makubaliano ya awali ya kushirikiana kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Ethiopia, Chuo Kikuu cha Port Harcourt (Nigeria) na Chuo Kikuu cha Joachim Chisamo (Msumbiji) katika kufundisha Kiswahili," alisema.

Mchengerwa alisema licha ya kuwa lugha ya kwanza kutoka Bara la Afrika, pia ni lugha yenye wazungumzaji wengi, wanaozidi milioni 200 duniani kote.

Alisema kutokana na kukua kwa lugha hiyo, Watanzania saba walipata nafasi ya kuhudumu katika mikutano mbalimbali ya Umoja wa Afrika (AU) na kamisheni zake, wakalimani wawili walihudumu katika Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika Februari, mwaka huu.

Kadhalika, wakalimani watatu na watafsiri wawili walihudumu katika Mkutano wa 71 wa Kamisheni ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Afrika uliomalizika Mei 13, mwaka huu.

Alisema kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Watanzania wengi wamenufaika na fursa za Kiswahili, inahitajika mikakati zaidi kuwekeza kueneza utafiti wa lugha.

"Wizara kupitia BAKITA imekamilisha maandalizi ya mkakati wa taifa wa kubidhaisha Kiswahili wa miaka 10 (2022- 2032), miongoni mwa maazimio yake makubwa unalenga kuwasajili wataalamu wa Kiswahili na kuimarisha stadi zao," alisema.

Alisema miongoni mwa wahitimu wapo waliomaliza madarasa ya ana kwa ana ya kufundisha Kiswahili kwa wageni na wengine wanafundisha kwa njia ya mtandao, na kwamba Kiswahili kwasasa ni bidhaa na ajira.

"BAKITA inaendelea kusajili wataalamu wa Kiswahili katika kanzidata ili Watanzania wengi zaidi watambulike utaalamu wao kipindi cha Julai, 2021 hadi Aprili, 2022 wamesajiliwa wataalamu 19 kati ya hao wanaume ni 13 na wanawake ni sita," alisema.

Mchengerwa alisema wataalamu waliosajiliwa ni 1,325, wanaalikwa Watanzania wote wanaojiamini na utaalamu mahsusi katika Kiswahili kutumia dirisha la BAKITA kujisajili ili wapate vyeti vitakavyowapa ajira duniani.




Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akikabidhi taulo za kike dazeni 50 kwa Mtangazaji wa East Africa Radio kipindi cha Mama Mia, Ritha Chuwalo, zilizotolewa na Kampuni ya The Guardian Ltd, Mikocheni , mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya wasichana wanaosoma kupitia kampeni ya Namthamini, inayoendeshwa na East Afrika Radio na EATV. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# The Guardian yatoa dazeni 50 kampeni 'Namthamini'

**Na Jenifer Gilla**

KAMPUNI The Guardian Limited imetoa msaada wa taulo za kike 5,000 kwa kampuni ya East Afrika Radio na Televisheni kuunga mkono juhudi za kampeni ya 'Namthamini' inayolenga kugawa pedi kwa wanafunzi ili kuwasaidia kuwa salama wanapokuwa kwenye hedhi.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe, alisema kuwa wametoa msaada huo ili kumsitiri mtoto wa kike anapokuwa kwenye hedhi.

"Tukiwa kama kampuni mama katika kampuni za IPP tumeona tuwaunge mkono wenzetu katika kampeni hii ili kumsaidia mtoto wa kike akiwa kwenye hedhi apate vifaa salama vya kumsitiri asishindwe kuhudhuria masomo," alisema.

Alisema wameguswa zaidi baada ya utafiti kuonyesha kuwa katika siku 28 watoto wa kike wanakosa masomo kwa siku nne kwa sababu ya kukosa vifaa salama wakiwa kwenye hedhi.

"Lakini ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu tunahitaji ushiriki sawa wa jinsia katika masuala muhimu ikiwamo elimu. Sasa hedhi salama imekuwa ni kikwazo kwa mtoto wa kike kuhudhuria shule na hapo ndipo pengo hilo linapoanza kuonekana kwa hiyo kwa kuchangia msaada huu tunaamini tunakwenda kuziba pengo hilo," alisema.

Meneja Uhusiano wa Wateja wa kampuni ya East Afrika ambaye ni Meneja wa mradi huo, Nancy Mwanyika, aliishukuru The Guardian kwa kuwapatia misaada hiyo na kusema kuwa mwaka huu wanategemea kuwafikia wasichana 5,000.

"Kwa niaba ya East Africa Television na Radio, tunapenda kuwashukuru The Guardian kwa sababu kila tukileta barua ya kuomba mtuunge mkono kampeni hii mara zote mmetuunga mkono na sio kwa kidogo, na hizi dazeni 50 zilizoletwa zitasaidia kuweka shule watoto kwa mwaka mzima," alisema Nancy.

Alisema wamekuwa wakigawa misaada hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa miaka sita sasa na kwa mwaka huu wanatarajia kuwafikia wasichana walipo kwenye mikoa ya Mtwara, Njombe na Ruvuma.

"Tunatamani kama tungeweza kupata pedi zaidi tungekwenda kwenye mikoa zaidi, uhitaji ni mkubwa, ni zaidi ya watoto 5,000. TAMISEMI wametupa idadi ya shule nyingi, lakini sasa tutaangalia na misaada tutakayopata kama itavuka malengo basi tutakwenda zaidi ya hapo," alisema.

Alitoa wito kwa watu na kampuni binafsi kuwaunga mkono katika kampeni hiyo kwa kidogo walichonacho ili kusaidia mtoto wa kike kuhudhuria masomo na kwa upande wa serikali kupunguza kodi katika bidhaa hiyo ili upatikanaji wake uwe rahisi.

"Kwa upande wa serikali tunaomba nao waweze kuangalia ni jinsi gani hizi bidhaa zinaweza kupatikana kwa urahisi zaidi, kwa sababu sasa hivi kuna suala la kodi kuwa kubwa. Kama tunavyojua mtoto wa kike kwenda hedhi ni maumbile na sio uchaguzi, wakati ukifika lazima atapata hedhi," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko tabia nchi tishio, tutunze mazingira

**KILA** Juni 5, ni maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo inalenga kuwakumbusha wanadamu umuhimu wa kutunza mazingira, kwa ajili ya kuondokana na uharibifu hatari kwao na viumbe wengine ambao wanategemea ikolojia kuishi.

Kwa sasa kasi ya uharibifu wa mazingira ni kubwa duniani na inachangiwa na shughuli za kibinadamu kama za viwanda, huku nchi zinazoongoza kwa uharibifu ni Marekani, China na Ulaya huku Afrika kwa ujumla wake ikichangia asilimia nne ya hewa ukaa.

Mkutano wa COP26 (Conference of Parties), ulijiwekea malengo ya kupunguza hewa ukaa kwa zaidi ya nusu ili kushusha joto kwa nyuzi joto 1.5, huku kila nchi ikitakiwa kuwasilisha mpango mkakati wake wa hadi 2030, na hadi sasa nchi 151 zimewasilisha, lakini nchi kubwa zinazochangia hewa ukaa kwa wingi hazijawasilisha.

Mathalani, Tanzania imejiwekea malengo ya kupunguza hewa ukaa kwa asilimia 30 hadi 35 ifikapo 2030, kwa kuwa na mipango kwenye sekta zote muhimu, hasa katika kulifikia lengo la kuondoa kabisa hewa ukaa ifikapo 2050.

Umoja wa Mataifa (UN), katika hesabu zao za makadirio ya mipango iliyopo na hatua zinazochukuliwa na nchi husika, inaona dunia itaweza kupunguza joto kwa nyuzi joto 2.5 ifikapo 2100.

Moja ya mikakati iliyopo duniani katika kupunguza uharibifu wa mazingira ni kuondoa matumizi ya nishati za gesi, mafuta na makaa ya mawe, kwa kuwekeza nguvu kwenye nishati jadidifu ambazo ni upepo, jua, upepo na mawimbi ya bahari na tungamotaka.

Tanzania ni moja ya nchi yenye rasilimali nyingi ya madini ya kimkakati ambayo zipo aina 17, ambazo zinahitajika sana duniani hasa katika kuzalisha nishati jadidifu, huku nchi zilizoendelea zikiwekea mkakati wa kuwa na mwongozo wa madini hayo.

Kwa ngazi ya nchi tunaweza kuweka mikakati mzuri ya kudhibiti mabadiliko ya tabia nchi, lakini mabadiliko ya tabia nchi hayabagui kwa kuwa uharibifu unaweza kufanyika Marekani na madhara ya kasambaa kote, licha ya kwamba Afrika inachangia kwa kiasi kidogo sana hewa ukaa, lakini ndiyo inayoathirika.

Kwa sasa tunaona mvua hazinyeshi kwa wakati, ukame wa muda mrefu na hivi karibuni tuliona mamia ya mifugo ilikufa wilaya za Loliondo, Manyara na Simanjiro, lakini maji yalipungua kwa kiasi kikubwa kiasi cha kuwa na mgawo wa maji na umeme, yote ni athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Hali ya upatikanaji wa chakula nao umeathiriwa kwa kiasi kikubwa, hivi karibuni Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilishauri wakulima wengi kulima mazao yanayohimili ukame na kuacha mazoea ya kulima mahindi, kwa kuwa hali ya ukame imezidi kuongezeka.

Kwa sasa kina cha maji Ziwa Tanganyika, Bahari ya Hindi na kwingine kinaongezeka kwa kasi, huku wananchi wa Pangani, Mafia na Micheweni Pemba wanaanza kumegwa na maji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kwa sasa shughuli za kilimo zimeathiriwa, mathalani kule Micheweni Pemba maji ya chumvi yamesababisha wakulima hawawezi kulima tena, huku wavuvi wakishindwa kuvua na maeneo ya mialo na huduma za kijamii yakimezwa na maji.


Suala la mabadiliko ya tabia nchi siyo jambo dogo linahitaji ushiriki wa dunia kulikabili, kama nchi tunaweza kuchukua hatua kwa uwezo wetu, lakini kuna nyingine ziko nje ya uwezo wetu.

Tuendelee kuhamasisha upandaji miti kwenye maeneo mengi, kuhamasisha wanakijiji kutunza misitu ili kuzalisha kaboni ambayo inauzwa duniani, lakini kutumia vyema fedha za mazingira zinazotolewa duniani zilionyesha mabadiliko kwenye maisha ya watu ili watunze mazingira.

Ni muhimu kuelimisha wananchi umuhimu wa kutunza mazingira, kushiriki moja kwa moja kuweka mazingira safi, mamlaka za serikali kusimamia sheria ipasavyo kudhibiti viwanda na kampuni zinazotiririsha kemikali ambazo ni hatari kwa wananchi.

Mathalani, ukienda maeneo ya mabondeni jijini Dar es Salaam, kuna kilimo cha mboga kinafanyika, lakini maji yanayotumika ni machafu hali ambayo ni hatari kwa afya za walaji, ni lazima kuwalinda wananchi dhidi ya maradhi mengine ambayo ni mzigo kwa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Nassir Nchimbi, TUDARCo

Muungwana Lazima Nilonge

# Taifa lisake chanzo ulawiti wa watoto

**INASIKITISHA** na kuudhi kusikia na kuona taarifa za watoto wanaolawitiwa kwenye jamii yetu.

Waathirika na familia zao wanasononeka kutokana na unyama wanaofanyiwa watoto na kuwasababishia maumivu makubwa kimwili, athari kisaikolojia na kuvuruga ustawi wao.

Matukio hayo yamekuwa mengi na kila wakati yamekuwa yakiongezeka, mbaya zaidi hata watoto wenye miezi sita wanadaiwa kufanyiwa ukatili huo.

Mathalani, Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi lilimkamata mwalimu wa mafundisho ya dini kanisani, huko Mpanda Mjini, Februari mwaka huu kwa tuhumu za kuwalawiti watoto wanne.

Kadhalika mwezi uliopita baada ya kuibua tuhuma za watoto wanane wenye umri kati ya miaka sita na nane kufanyiwa ukatili wa kingono na mwalimu wao katika shule moja ya msingi iliyopo Kinondoni Dar es Salaam.

Taarifa hizo zilitolewa siku saba baada ya uchunguzi wa kina wa tukio hilo kufanyika.

Haya ni baadhi ya matukio ya karibuni yaliyoripotiwa tena katika mazingira ambayo jamii inayaamini kuwa watoto wapo salama shuleni kwenye uangalizi wa walimu.

Walimu wanaaminika tena wanachukuliwa kuwa ndiyo walimu na viongozi wa watoto wakiwa nje ya familia zao au kwenye mikono ya wazazi na walezi.

Ripoti hizo za polisi zinaweza kuondoa imani ya jamii kwa wahusika ambao walikabidhiwa watoto, kama sehemu ya umma wa Watanzania wakishangaa kuwa inakuwaje walimu wanajihusisha na ukatili huo kwa watoto.

**Taarifa hizo zilitolewa siku saba baada ya uchunguzi wa kina wa tukio hilo kufanyika.**

Vitendo ambavyo vinabadilisha maisha ya watoto wa kiume na wa kike na kuwasababishia kuwa 'viumbe' wasiokubalika ndani ya jamii kutokana na matendo yanayohusishwa na 'Sodoma na Gomora'.

Miji hiyo inatajwa katika maandiko matakatifu kuwa ilichomwa na moto wa Mungu kutokana na matendo ya ulawiti.

Walimu, wazazi na hata viongozi wa taasisi za kidini wanatakiwa kukemea uovu huo.

Kama walivyo wengine nami najiuliza jamii yetu inaelekea wapi? Suluhu ya haya majanga ni nini? Je, wazazi na walezi tufanye nini kuwalinda watoto wetu, au tumekwama wapi mpaka wanakumbana na matatizo hayo?

Hakuna mlezi au mzazi asiyemlinda mwanawe, juhudi zinafanywa kuwalinda watoto wetu, lakini wahalifu nao wamekuwa na mbinu nyingi ambazo zimekuwa hatarishi zaidi.

Mfano mwalimu wa dini huko Katavi, anadaiwa kabla ya kuwalawiti watoto hao wanne, alikuwa akiwalaghai wamsindikize kwenda kufanya shughuli za kibiashara sehemu tofauti.

Anadaiwa alikuwa anawabeba kwenye pikipiki yake baada ya kumaliza vipindi vyao vya masomo.

Inasikitisha mno, lakini yameshatokea kikubwa ni kudhibiti matendo hayo kwa kuanza na malezi kwa vijana wetu wakiume ambao ndiyo baba wa taifa la kesho.

Ni lazima kuwafundisha kuhusu ubaya na athari za ulawiti ili wakue wakiwa walinzi wao wenyewe na wa dada zao.

Ili hapo baadaye waendelee kuwa walinzi wa wao wenyewe kama watoto wa kiume, dada zao, wadogo zao na jamii nzima.

Wazazi na walezi kwa upande wao wana jukumu la kuhakikisha mienendo ya watoto wao pamoja na watu au wafanyakazi wanaowaachia kuwangalia ama kuwalea.

Ni muhimu kuwa makini nao na kuwachunguza kutokana na ukweli kuwa walezi (yaya) wengi ndiyo watu wanaotuhumiwa na kesi zinazoripotiwa polisi za kuwalawiti watoto.

Kwa upande wa serikali sheria kali zinahitajika kwa wanaokutwa na hatia ya ulawiti, pengine zilizoko zimekuwa nyepesi ndiyo maana vitendo hivi vya kikatili vimekithiri.

Ni wakati wa kusimama na kutazama nyuma taifa likijipanga tena kudhibiti udhalimu huo.

## Teknolojia kuchakata taarifa wakopaji yabuniwa

**Na Gwamaka Alipipi**

TAASISI ya Dun & Bradstreet Bureau Tanzania, imezindua teknolojia ya EDX yenye uwezo wa kuchakata, kusafirisha na kuwasilisha taarifa, maalum kwa taasisi za fedha ziweze kuwasilisha taarifa za wakopaji kwenda kwenye kanzi data ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa teknolojia hiyo, Meneja wa taasisi hiyo, Junaid Malik, alisema itazisaidia taasisi za kifedha kuondoa makosa wakati wa uwasilishaji wa taarifa hizo, kuokoa gharama pamoja na kutoa taarifa sahihi pale zinapohitajika.

"Ni teknolojia ambayo hurahisisha uchakataji na uwasilishaji wa taarifa za wakopaji kwa taasisi za kifedha kwa njia ya kielektroniki. Vilevile, uwasilishaji wa taarifa za wakopaji kwa njia hii ya kisasa utarahisisha mtiririko wa kazi kwa taasisi husika, kupunguza makosa pamoja na kusaidia taasisi kufuata kanuni na sheria za BoT za ukusanyaji wa taarifa za mikopo," alisema Malik.

Malik alisema teknolojia ni moja ya nguzo kuu kwa taasisi za kifedha na benki, uwapo wa teknolojia hiyo umesababisha kuongezeka kwa idadi ya taarifa zinazohifadhiwa, usimamizi pamoja na ongezeko la mahitaji ya taarifa kutoka kwa wasimamizi wa sekta ya fedha.

Malik alisema EDX inasaidia kuokoa gharama za uendeshaji kwa zaidi ya asilimia 75 pia ni rahisi na haraka kuunganisha na inachukua muda mfupi usiozidi wiki tatu, huku miundombinu yake ikichukua nafasi ndogo.

Alisema pia inasaidia kufikia vyanzo vingi vya taarifa, kuwasilisha, kuhakiki na kuchapisha kwenye muundo wowote, inapunguza uingizaji wa data kwa mkono kwa asilimia 90, kutoa taarifa kwa wakati na kupunguza kupoteza muda kwa zaidi ya asilimia 85.



**Malik alisema teknolojia ni moja ya nguzo kuu kwa taasisi za kifedha na benki, uwapo wa teknolojia hiyo umesababisha kuongezeka kwa idadi ya taarifa zinazohifadhiwa, usimamizi pamoja na ongezeko la mahitaji ya taarifa kutoka kwa wasimamizi wa sekta ya fedha.**

# DC aagiza mwalimu anayedaiwa kumnajisi mwanafunzi akamatwe

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MKUU wa Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, Paul Chacha, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani humo kumkamata mwalimu wa Shule ya Sekondari Igwisi, Aristides Mushi kwa tuhuma za kumnajisi mwanafunzi wa kidato cha pili.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari na kubainisha kuwa mwalimu huyo alimlaghai mwanafunzi wake (jina limehifadhiwa) na kumpeleka porini kisha kumfanyia unyama huo.

Alisema kitendo hicho hakikubaliki na ni kinyume cha maadili ya utumishi wa umma, hatua za kisheria ni lazima zichukuliwe.

Chacha alisema amemsimamisha kazi Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Rose Nzingo kwa madai ya kushindwa kumchukulia hatua mwalimu huyo ambaye anadaiwa kuhusika na matukio kadhaa ya udhalilishaji wa wanafunzi kingono shuleni hapo.

Alisema mwalimu huyo anatuhumiwa kuwalazimisha watoto wa kike na wa kiume kuvua nguo na kufanya nao matendo ya kingono ofisini kwake, huku akiwapiga picha kwa kutumia simu yake ya kiganjani.

"Vitendo vya namna hii havikubaliki ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu sana kwa mwalimu kumbaka au kumfanyia mwanafunzi vitendo vyovyote vya kingono, huu ni udhalilishaji, hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa ili kukomesha tabia hii," alisema Chache.

Awali, Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Rose alikiri kuwapo kwa tuhuma zinazomhusisha mwalimu huyo wa nidhamu na kubainisha kuwa walikuwa wameshamwonya, lakini hakusikia.

Ofisa Elimu Sekondari wilayani humo, Daud Nkwanu, alisema wamepokea maelekezo ya Mkuu wa Wilaya na sasa wameanza uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili mwalimu huyo kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Akizungumza kwa niaba ya wazazi, Said Juma, ambaye ni mkazi wa Igwisi aliomba hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya mwalimu huyo ili kukomesha vitendo hivyo.



Msururu mkubwa wa magari yakipita katika barabara ya mchepuko, kutokana na kuendelea kwa ujenzi wa daraja la magari na treni, eneo la Puma Kurasini, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jela miaka 10 kutapeli mil. 27/- kwa simu

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, imemhukumu kwenda jela miaka 10 mkazi wa Mkuti wilayani Masasi, mkoani Mtwara, Mohamedi Rashidi, kwa kukutwa na kosa la utapeli wa jumla ya Sh. milioni 27.5 kwa njia ya simu kupitia wakala wa huduma za fedha.

Mshtakiwa alihukumiwa kifungo hicho baada ya kukiri kutendo kosa hilo na kwa kuwa hakuwa na la kujitetea alikubali kwenda jela miaka 10.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Mahakama ya Wilaya ya Masasi na Hakimu Batista Kashusha.

Upande wa serikali ulidai mahakamani kuwa mashtakiwa alitenda kosa hilo Mei 31, mwaka huu, kwa mfanyabiashara wa huduma za fedha ambaye ni wakala wa kuweka na kutoa fedha wa Benki ya CRDB wilayani humo.

Ulidai mahakamani hapo kuwa, mshtakiwa huyo alimtapeli Ashura Nassoro, wakala wa huduma za fedha mkazi wa Mtaa wa Mkuti wilayani Masasi Sh. milioni 17.5.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitumia njia ya simu kufanya utapeli huo na kujipatia kiasi hicho cha fedha kwa manufaa yake binafsi.

Pia, ulidai mshtakiwa huyo kwa kipindi cha nyuma mwaka 2021, alishakuwa na kesi kama hiyo ya utapeli wa Sh. milioni 10 kwa mmoja wa wakala wa huduma za fedha.

Mshtakiwa alipoulizwa mahakamani kuhusu makosa hayo aliyoyatenda mbele ya hakimu huyo, alikiri.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kashusha alisema kuwa kwa vile mshtakiwa amekiri makosa yake, mahakama inampa adhabu ya kifungo cha kwenda jela miaka 10.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea alisema kuwa hakuwa na cha kujitetea na kukubali kwenda kutumikia kifungo hicho jela.

# Kesi meno tembo inayomkabili raia wa Guinea yashindwa kusikilizwa

**Na Grace Gurisha**

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili mfanyabiashara Ally Anguzuu, raia wa Guinea na wenzake 10 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeshindwa kuendelea kwa sababu ya wakili wa mshtakiwa wa pili, Josephat Mabula, kutofika mahakamani.

Washtakiwa wengine ni mfanyabiashara Victor Mawala, Haruni Abdallah, Abbas Hassan, Solomoni Mtenya, Khalfani Kahengele, Ismail Kassa, Juma Buguma, Kassim Saidi, Peter Nyachiwa, John Buhanza na Mussa Abdallah wote wakazi wa Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Janeth Magoho alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga kuwa kesi hiyo ilikuja kwa ajili ya kusikilizwa na wapo tayari kuendelea.

Magoho alidai mara ya mwisho mshtakiwa Mawala alieleza mahakama kuwa wakili wake (Mabula) alishindwa kufika mahakamani kwa sababu ana kesi nyingine Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi na kwamba alikataa mawakili wenzake kuendelea na kesi hiyo hadi awepo.

Hata hivyo, mshtakiwa aliiomba mahakama azungumze na wakili wake kama ataridhia mawakili wenzake kuendelea na kesi hiyo kwa sababu yeye ndiye aliyekataa kuendelea kwa kesi hiyo.

Hakimu Ngimilanga alimtaka mshtakiwa kufanya mawasiliano na wakili wake ili kujua kama waendelee kusikiliza kesi hiyo bila uwepo wake kwani bila hivyo, itasababisha kuahirishwa kwa kesi mara kwa mara.

Hakimu Ngimilanga aliahirisha kesi hiyo hadi Juni 8, 9 na 10 mwaka huu kwa ajili ya kuendelea na usikilizaji.

Washtakiwa katika kesi hiyo wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, ambazo ni meno hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Wanadaiwa kuwa na mtandao mkubwa wa uhalifu wa ujangili ambao unajihusisha na kuuza na kununua, kupokea na kuhamisha, kusafirisha nyara za serikali ambazo ni meno ya tembo.



Makamu Mkuu wa Chuo cha Kilimo na Mifugo Kaole Wazazi cha Bagamoyo, mkoani Pwani, Maximillian Sarakikya (watatu kulia), akifafanua jambo kwa baadhi ya wafanyakazi wa kampuni ya bia ya Serengeti (SBL), waliotembelea chuo hicho mwishoni mwa wiki. Wengine ni wanafunzi wa chuo hicho ambao ni wanufaika na programu ya ufadhili wa masomo inayojulikana Kilimo Viwanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC akumbana na kilio cha ukosefu wa maji salama

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kijiji cha Makowo, Kata ya Makowo Halmashauri ya Mji wa Njombe, wamesema uhaba wa majisafi na salama umewasababishia baadhi yao kufunga kuzaa kwa kukosa huduma hiyo.

Waliyasema hayo katika mkutano wa Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alipofika kusikiliza kero za wananchi.

Walisema wanawake wana uhitaji mkubwa wa maji, lakini uhaba huo umewasababishia baadhi yao kufunga uzazi.

Mmoja wa wakazi hao, Prisca Mligo alisema: "Unakuta hata kuzaa kinamama wamefunga kwa sababu ndoo moja ya maji inabidi uitumie kwa matumizi mengi, ufue nguo za watoto, upikie, unywe kwa kweli kilio cha sisi wamama ni maji, kata yetu ina vyanzo vingi vya maji, lakini hatujui tatizo linatoka wapi."

Christopher John kwa upande wake alisema wanawake wa kijiji hicho wanatoka shambani wakiwa wamebeba watoto mgongoni, wakirudi nyumbani inabidi wakatafute maji.

Naye Diwani wa Kata ya Makowo, Pilimini Mgaya, alisema tatizo la maji katika kijiji hicho ni la muda mrefu.

"Suala la maji Makowo ni tatizo kubwa na vilevile ukiangalia kituo cha afya kinahitaji maji mengi, kati ya vitongoji sita ni viwili tu ndivyo vinapata maji," alilalamika.

Akizungumzia tatizo hilo, Mhandisi Bakari Kitogota kutoka RUWASA alisema mpango uliopo ni kutembelea vyanzo vya maji ili kutatua tatizo hilo na kwamba maji yapo isipokuwa hayatoshelezi. Mkuu wa Wilaya ya Njombe, ameanza ziara ya kutembelea wananchi kijiji kwa kijiji, lengo kusikiliza kero kila kona ya wilaya yake.

Alisema hadi sasa ameshazifikia kata za Iwungilo, Lugenge pamoja na Makowo.

**Naye Diwani wa Kata ya Makowo, Pilimini Mgaya, alisema tatizo la maji katika kijiji hicho ni la muda mrefu.**

# Wakazi Bariadi walalamika uhaba wa mafuta

**Happy Severine,** BARIADI

ZIKIWA zimepita siku kadhaa tangu serikali kutangaza kushuka kwa bei ya mafuta nchini, wananchi wa mji wa Bariadi mkoani Simiyu wamedai nishati hiyo kuwa adimu.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi hao Yusuph Juma, dereva wa magari madogo, alisema tangu Jumatatu mafuta hayapatikani na vituo vyote vya mjini havitoi huduma hiyo.

Alisema kuwa vituo vyote vya mafuta havitoi huduma na kudai wamiliki wameficha kutokana na kutangazwa kushuka kwa bei.

"Tunahangaika kutafuta mafuta...na kwa sasa tuko hapa kwenye kituo hiki cha Fantom tunanunua kwa foleni kubwa...vituo vingine haviuzi kabisa na hatujui sababu ni nini," alisema Juma.

Mkazi mwingine wa Bariadi, Cosmas Edward, alisema suala la mafuta hususan ya dizeli yanapatikana kwenye vituo vichache nje ya mji na vilivyoko mjini haviuzi kwa madai kuwa yameisha.

"Tumeamka toka asubuhi tuko kwenye foleni na tunasubiria mafuta hapa Fanton, sehemu zingine haziuzi na hatujui sababu hasa ya wao kutouza mafuta hayo," alisema Edward.

Nipashe ilizungumza na mmoja wa wamiliki wa vituo vya mafuta vya JBS Fuel, John Sabu, alisema tatizo la kutopatikana mafuta katika vituo vyake lipo, lakini limetokana na yeye kuchelewesha kutuma magari ya kuleta kutoka Dar es Salaam hadi Bariadi na yaliyokuwapo yamekwisha.

Sabu aliwataka wananchi kuwa watulivu na kuahidi ndani ya muda wa siku mbili mafuta yatakuwa yamefika na utoaji huduma hiyo kwenye vituo vyake utaendelea kama kawaida.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lusakisyo Kapange, alisema kuwa suala la kutokuwapo kwa mafuta Bariadi sio la kweli na kuwa amezunguka katika vituo vyote vilivyoko mjini na kukuta nishati hiyo. Aliwasihi wananchi kupuuzia uzushi wa wachache wanaovumisha kuwa mafuta yamefichwa.

HABARI KITAIFA

## Ndaki awataka wafugaji, wavuvi kuhifadhi mazingira

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewataka wafugaji na wavuvi nchini kuhifadhi mazingira kama njia pekee ya kuziwezesha sekta za mifugo na uvuvi kuwa endelevu katika kujipatia kipato na kukuza pato la taifa.

Ndaki alitoa wito huo baada ya kutembelea mabanda katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma Juni 5, 2022.

Alisema shughuli za ufugaji na uvuvi zina uhusiano mkubwa na utunzaji na uhifadhi mazingira na ndiyo maana wizara inawasisitiza wafugaji na wavuvi kuendelea kuhifadhi mazingira ili kufanya malisho ya mifugo yaendelee kuwa mengi na mazalia ya samaki yaweze kuwa endelevu na kutoa mazao ya kutosha.

"Sisi wizara tunazuia kabisa wavuvi kufanya uvuvi katika matumbawe ambayo ndio kiwanda cha kuzalisha samaki ili tuendelee kuwa na uvuvi endelevu na wenye tija kwa taifa," alisema.

Kadhalika, alisema ili mifugo iwe na ustawi inategemea uwapo wa malisho na maji ya kutosha na ndiyo maana wanahimiza wafugaji kutunza nyanda za malisho na vyanzo vya maji ili ufugaji uwe na faida kwa wafugaji na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Kitengo cha Mazingira, Sekta ya Uvuvi, Melton Kalinga, alisema utunzaji wa mazalia ya samaki ni muhimu kwa uvuvi endelevu, pia ni moja ya vivutio vikubwa kwenye sekta ya utalii nchini.

Naye, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mazingira, Sekta ya Mifugo, Yusuph Selenge, alisema ni muhimu kuhifadhi mazingira kwa kuvuna na kuhifadhi malisho kwa kuwa kufanya hivyo kunasaidia kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi huku akiongeza kuwa ni muhimu wafugaji kuzuia mifugo yao kuzagaa ovyo kwa sababu ni chanzo cha uharibifu wa mazingira.

Kwa upande wake Balozi wa Mazingira nchini na Mwandishi wa Habari, Oliver Nyariga, alisema ni muhimu kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya afya ya jamii na kuepusha magonjwa mbalimbali yanayoweza kusababishwa na uharibifu wa mazingira.

Naye Miss UDOM mshindi wa tatu, Agnes Budeba, aliwaomba wavuvi hususan wanaofanya shughuli zao katika ukanda wa Ziwa Victoria kufanya uvuvi endelevu na tija kwao na taifa kwa ujumla.

# Waziri aeleza umuhimu wa elimu teknolojia ya maabara

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, amesema kuwa elimu zaidi inahitajika katika teknolojia ya maabara kuongeza thamani ya bidhaa zinazopatikana nchini ili kumudu ongezeko la uhitaji wa bidhaa kutoka kwa watumiaji na soko la kimataifa.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, katika ufunguzi wa mkutano wa siku mbili wa Teknolojia ya Maabara ya Ujerumani kwa Tanzania, ulioandaliwa na Wizara ya Masuala ya Uchumi na Ulinzi wa Hali ya Hewa ya Shirikisho la Ujerumani (BMWK) kwa kushirikiana na Ujumbe wa Viwanda na Biashara wa Ujerumani kwa Afrika Mashariki, kupitia Chama cha Viwanda na Biashara cha Ujerumani (AHK).

Aliyataja baadhi ya maeneo yanayohitaji teknolojia hiyo kuwa ni kilimo na usindikaji wa vyakula, migodi, ujenzi na barabara, mafuta na gesi, wiwanda na dawa.

"Kama mnavyojua uhitaji ni mkubwa hapa Tanzania, tunatumia pesa nyingi kuagiza dawa kutoka nje kwa hiyo tunahitaji teknolojia ili tuweze kujitegemea na kuvumbua pamoja fursa zinazopatikana katika uwekezaji wa sekta ya dawa," alisema.

Alisema ni dhahiri kuwa dunia imekuwa na ushindani, ili nchi iwe na uhimilivu katika biashara na kuongeza uhitaji kufanya utafiti, teknolojia na uvumbuzi na teknolojia ya maabara ni sehemu ya mlolongo huo.

Alisisitiza ushirikiano wa teknolojia hiyo uendelee kuimarika ili kampuni kutoka nchi hizo mbili zibadilishane ujuzi kukuza teknolojia hiyo nchini kwa lengo la kufikia ushindani wa kimataifa.

"Kwa hiyo ninategemea kusikia washiriki kutoka wawekezaji kutoka Tanzania na Uganda, tuongelee kuhusu biashara, tuongee kuhusu teknolojia na ugunduzi kwa maendeleo ya nchi zetu," alisema.

Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alisema Tanzania ni soko muhimu kwa Ujerumani na ujumbe toka kampuni saba zitaonyesha maabara zao, huduma na suluhisho kwa sekta binafsi na taasisi za umma.

"Kuna fursa zaidi hivyo kampuni zinatafuta soko, kuboresha mauzo ya biashara zilizopo au baadhi yao kuingia katika soko la uhakika," alisema.

Dk. Fadi Younid, mwakilishi wa kampuni ya Kijerumani, Analytik Jena GmnH, alisema Tanzania ilikuwa muhimu kwa kampuni za Ujerumani zenye utulivu, ukuaji wa haraka na uchumi wa afya.

"Tanzania inahitaji teknolojia hivyo ni sehemu sahihi ya kuwekeza kwenye teknolojia ya maabara. Tumechagua hapa kuwa makao makuu cha kampuni zetu tutakazofungua katika nchi za Jangwa la Sahara," alisema.

Naye Dk. Christian Zankiewics kutoka dawati la nchi za Jangwa la Sahara alisema, Ujerumani inaiona Tanzania na nchi nyingine za Afrika kama sehemu ya fursa na uhusiano wa kibiashara katika nchi hizo mbili umekuwa hadi asilimia 18 kufikia mwaka 2018.

Aliongeza kuwa kwa sasa Tanzania na Kenya zinatoa fursa kubwa kutoa uwezo mkubwa wa teknolojia ya Kijerumani ya uchambuzi wa kibiolojia na maabara na kuwa bidhaa na suluhisho za nchi hiyo hasa katika uwanja wa vifaa maalum na utumiaji huzingatiwa na zinahitajika wakati na nchi hizo ndiyo zenye nguvu zaidi kiuchumi katika nchi za Jangwa la Sahara.

Katika mkutano huo, ujumbe wa kampuni saba kutoka Ujerumani zilionyesha teknolojia zao za maabara, huduma na suluhisho kwa madhila zaidi ya kampuni mia moja za kitanzania.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akipata maelezo kuhusu uandaaji na uhifadhi wa malisho ya mifugo na Ofisa Mifugo Mkuu, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (Sekta ya Mifugo), Deograsias Ruzangi, alipotembelea banda la maonyesho la Wizara ya Mifugo na Uvuvi yaliyofanyika katika Viwanja vya Jakaya Kikwete, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msimu kilimo kuzinduliwa H'shauri Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama imesema itazindua rasmi mpango wa kilimo wa mwaka 2022/2023 katika Halmashauri ya Ushetu mwezi huu kwa kuwa na maeneo mazuri ya ardhi yenye rutuba katika kuwaandaa wakulima kutekeleza mpango mkakati wa kuwasaidia uzalishaji kwa tija mazao ya chakula na biashara.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Tawala wa Wilaya, Timoth Ndanya kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Festo Kiswaga, wakati akifungua mafunzo ya wajasiriamali wasindikaji na wafungashaji wa mchele, yaliyotolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ya kuwapa elimu ya umuhimu wa kufunga kwa ubora bidhaa na kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Ndanya alisema, katika mkakati huo kabambe wa wilaya wa kuzindua msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023 utakaozinduliwa mwezi huu, huku Benki ya Equity wilayani hapa ikiwa tayari kuwasaidia wakulima kuwakopesha mikopo ya kilimo yenye masharti na riba nafuu waweze kuzalisha kwa tija.

Alisema, Wilaya ya Kahama ina maeneo mazuri ya ardhi kubwa yenye rutuba kwa kilimo na serikali inataka kuona wakulima wanaitumia kuzalisha kwa tija katika mazao mbalimbali ya chakula na biashara badala ya kutegemea tumbaku na pamba wanaweza kuongeza zao jingine la alizeti.

Vile vile, alisema dunia ya leo bila kuwa na bidhaa zenye kiwango cha ubora huwezi ukapata soko zuri la ndani na nje ya nchi na kuwataka kuzingatia elimu wanayopewa na Shirika la Viwango Tanzania, kutengeneza bidhaa na kuzifunga pamoja na umuhimu wa kuwa na nembo ya ubora toka shirika hilo.

Naye Ofisa Udhibiti Ubora Mwandamizi wa TBS, Dk. Joseph Mwashiuya, alisema katika utafiti waliofanya kuhusu usindikaji na ufugashaji wa mchele kwa wajasiriamali wilayani hapa, walibaini kuwapo kwa kasoro nyingi na kuamua kuwapatia mafunzo waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na kiwango kinachotakiwa sokoni.

Alisema, wajasiriamali wengi wanazalisha bidhaa zenye ubora unaohitajika sokoni, lakini hawana elimu ya ufungaji wa bidhaa hizo na badala yake wanafunga kienyeji na kuchangia kuendelea kukosa masoko ya nje na kutegemea soko la ndani ya nchi pekee.

Mmoja wa wajasiriamali walioshiriki semina hiyo, Neema Mussa, aliipongeza shirika hilo kwa kuwapatia elimu ya namna ya kusindika na kufungasha kwa ubora bidhaa wanazozalisha na kwamba hali hiyo itawafanya kupata masomo ya nje ikiwamo Uganda, Rwanda, Kongo pamoja na Burundi.

Mshiriki mwingine, Alfa Mwaluseke, alisema elimu ya ufungaji wa bidhaa aliyoipata atamsaidia kuwaelimisha wajasiriamali wengine ambao hawakupata nafasi ya kushiriki na lengo likiwa ni kuzalisha na kufunga bidhaa katika vifungashio vinavyohitajika ili kuendelea kuitangaza Tanzania katika soko la dunia.

Hivi karibu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Equity nchini, Betty Kwoko, alipokuwa akizindua tawi wilayani hapa, alisema anaunga mkono mpango wa serikali katika suala la kilimo na watawasaidia wakulima kuwapatia mikopo ya kilimo yenye riba nafuu, wajasiriamali, wafanyabiashara wadogo na wakubwa waweze kuinuka kiuchumi na kuchangia pato la taifa.

# Serikali kuangalia adhabu mbadala kupunguza msongamano magereza

BUNGE limeelezwa kuwa kipaumbele cha serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 ni kufumua na kupanga upya mfumo wa jinai ikiwamo kuangalia adhabu mbadala ili kupunguza msongamano kwenye magereza.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Felister Njau, aliyehoji serikali haioni haja ya kuja na adhabu mbadala ili kupunguza msongamano huo.

Alisema kuna kero kubwa ya msongamano wa mahabusu na wafungwa kwenye magereza kukithiri.

"Je, serikali inaonaje ikaleta utaratibu wa vifungo vya nje kwa makosa madogo madogo ili kupunguza msongamano huo," alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Ndumbaro alisema mbali na mpango huo, pia kukamilika kwa mfumo wa anwani za makazi utawafanya watuhumiwa kujidhamini wenyewe na kupunguza hali hiyo.

Alisema wakati wa kupitisha bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2022/23, moja ya vipaumbele ni kwenda kuangalia upya, kuufumua na kuupanga upya mfumo wa jinai hapa nchini.

"Moja ya jambo ni kuangalia adhabu mbadala ambazo zitasaidia kupunguza msongamano wa mahabusu kwenye magereza," alisema.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, alitaka kujua ni lini serikali itawasilisha muswada wa sheria unaozuia polisi kukamata na kuwashikilia watuhumiwa kabla ya kukamilisha upelelezi.

Katika swali lake la nyongeza, Kingu alihoji idadi kubwa ya mahabusu walioko kwenye magereza kuipa mzigo mkubwa serikali kuwahudumia.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kuleta sheria itakayowezesha watuhumiwa kupewa nafasi ya kujidhamini wenyewe ili kuipunguzia mzigo serikali na kuwapunguzia adha Watanzania wanaoteseka magerezani," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Dk. Ndumbaro alisema lengo la kumdhamini au kujidhamini kwa mtuhumiwa kurudi mahakamani kwa tarehe iliyopangwa na kusisitiza kuwa kukamilika kwa mfumo wa anwani za makazi kutawezesha kutambua anapoishi.

"Lengo la mtuhumiwa kudhaminiwa au kujidhamini ni kuhakikisha anarudi mahakamani kwa tarehe iliyotakiwa, kwa hivi sasa serikali imejikita katika mpango wa kuweka anwani za makazi pindi zoezi hili litakapokamilika tutakuwa na uwezo wa kujua nani anaishi wapi hivyo kutakuwa na uwezekano wa kujidhamini wenyewe," alisema.

"Kwa hiyo kazi ambayo Mheshimiwa Nape (Nnauye) anaifanya ikikamilika pamoja na Vitambulisho vya Taifa Watanzania watajidhamini wenyewe hivyo kupunguza msongamano wa mahabusu ambao watakuwa wako nje."

Kadhalika, alisema serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20 kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba moja ya waka 2022.

"Kwa sasa sheria imeweka masharti ya kutofungua mashtaka mpaka upelelezi utakapokamilika, isipokuwa kwa makosa makubwa tu," alisema.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akijadiliana jambo na Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamadi Masauni, Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Sheria zinazokinzana umiliki ardhi zipitiwe upya'

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, ametaka mpango wa serikali wa kupitia sheria zinazokinzana na sheria namba nne na tano juu ya umiliki wa ardhi kwa wanawake na watoto wa kike.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alisema kwa mujibu wa takwimu za serikali za mwaka 2016 asilimia 19 pekee ya wanawake ndiyo wanamiliki ardhi licha ya kuchangia asilimia 54 ya uzalishaji kwenye kilimo.

"Je, serikali imeweka kipaumbele gani kuhakikisha kwamba umiliki wa ardhi wa wanawake unaongezeka kwa kuipa uhai na meno sheria namba nne na tano," alihoji.

Alisema mila, tamaduni na desturi ni miongoni mwa sababu kubwa zinazochangia umiliki wa ardhi kwa wanawake.

"Je, serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba sheria za kimila za umiliki ardhi pamoja na sheria zingine ambazo zinakinzana na sheria namba nne na tano haziwi juu ya hii sheria mama ya umiliki wa ardhi wa sheria namba nne na tano," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kwa mujibu wa Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inampatia kila mtu bila kujali jinsia yake, haki ya kumiliki mali ikiwamo ardhi na haki ya hifadhi kwa mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria.

"Kufuatia masharti ya Katiba, Sera na Sheria za Ardhi, Tanzania ina umiliki sawa wa ardhi kwa mwanaume na mwanamke," alisema.

Hata hivyo, alisema kama kuna sheria inayokinzana na Katiba na Sheria za Ardhi namba nne na tano kuhusu umiliki wa ardhi kati ya mwanaume na mwanamke, serikali itaanzisha mchakato wa kuzifanyia mabadiliko sheria hizo.

"Umiliki wa ardhi kwa watoto chini ya miaka 18 ni kupitia waangalizi wao kwa mujibu wa sheria," alisema.

Dk. Ndumbaro alikiri kuwa idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi Tanzania bado ipo chini na haisababishwi na sheria bali mtazamo wa jamii, mila na desturi ambazo sasa ni lazima serikali ishirikiane na wadau kutoa elimu kuhusu haki ya mwanamke kumiliki ardhi kwa mujibu wa Katiba.

"Sheria za kimila zimekuwapo tangu zamani ni wazi zinakinzana na haki za wanawake ambazo zimeelezwa kwenye Katiba na kikataba mingine ya kimataifa ambayo tumesaini sisi kama serikali tumejipanga kupitia sheria hizi ili kupendekeza mabadiliko na endapo Bunge litaridhia basi tutaondoka katika kadhia hii," alisema.

# Waziri aondoa utata maombi elimu nje ya nchi

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia imeliambia Bunge kuwa nafasi za masomo nje ya nchi hutolewa bila kujali mwombaji anatoka upande upi wa Muungano.

Naibu Waziri wa Elimu, Omar Kipanga alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji vijana wangapi wa Tanzania wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kwa mwaka 2015-2020 na kati yao ni vijana wangapi kutoka Zanzibar wamepata nafasi hizo.

Akijibu swali hilo, Kipanga alisema Watanzania walionufaika na ufadhili wa masomo nje ya nchi ni 856 na kati yao wanaume ni 609 sawa na asilimia 71.1 na wanawake 247 sawa na asilimia 28.9. Alisema nafasi za ufadhili wa masomo nje ya nchi huratibiwa kwa ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano kupitia Idara zinazosimamia Elimu ya Juu.

"Idara hizo zina jukumu la kubainisha sifa za waombaji na kupendekeza wanufaika wa ufadhili husika pasipo kujali mwombaji anatoka upande upi wa Muungano," alisema.

Alisema zipo baadhi ya nafasi za ufadhili wa masomo ambazo huratibiwa moja kwa moja na nchi au shirika linalofadhili.

Alisema kwa mwaka 2015 hadi 2021, wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, iliratibu ufadhili wa masomo katika nchi za Uingereza, Hangaria, China, Morocco, Misri, Algeria, Urusi, Ujerumani, Msumbiji, Thailand, Mauritius, Iran na Indonesia. Katika swali lake la nyongeza, alihoji huduma za vijana hao kutoka Zanzibar hadi chuoni.

"Vijana wanaoteuliwa kwa asilimia kubwa ni wanaume kuliko wanawake na wanawake kipindi hiki wanachacharika kupata elimu, je, mtizamo huo upo kwa namna gani hadi wanawake wanakuwa kidogo," alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Kipanga alisema ufadhili kwa vijana hao wanaokwenda nje unafanywa na nchi husika ambazo wanafunzi hao wanakwenda.

"Ingawa sisi serikali tumetoa fursa kwa Bodi ya Mikopo kuwa na ufadhili ambapo kuna wanafunzi wanafadhiliwa kupitia Bodi hiyo ya Zanzibar na Tanzania Bara," alisema.

Alikiri idadi ya wanaume ni kubwa kuliko wanawake na kwamba inatokana na sifa ambazo zinatakiwa kwenye vyuo hivyo wanavyokwenda kusoma ikiwamo kuangalia ufaulu.




Habari zote na Augusta Njoji



Ukurasa 12

‘Uwezo Award’ tuzo inayopika wanafunzi kuwa wajasiriamali

Nipashe
TESA
Jumanne Juni 7, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

**Kilio taulo za kike wadau watamani ‘pedi za kudumu’**

ELIMU

MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Manusura wa ndoa utotoni asherehekea kuwa darasani

• Anatamani ualimu na kuinua familia yake

MWANAFUNZI aliyenusurika kuozwa muda mfupi baada ya kumaliza darasa la saba na kufaulu kwenda sekondari, akilipiwa mahari ya ng’ombe 14, yuko shuleni baada ya juhudi binafsi za kukataa ndoa za udogoni kuzaa matunda.

Binti huyo, jina tunalo anasoma katika Sekondari ya Mwangulumbi, mkoani Shinyanga, alihitimu elimu ya msingi, nyumbani kwa mama yake anayeishi katika Kijiji cha Sayu wilayani Shinyanga.

Mtoto huyo, alilazimishwa ndoa baada ya baba yake kufanya maandalizi, akimpatia mchumba anayedaiwa alimkabidhiwa ng’ombe 14 na mali nyingine.

**ALIVYONUSURIKA**

Binti huyu mwenye miaka 15 alifaulu kwenda Sekondari ya Pandagichiza mkoani Shinyanga, lakini kabla ya kuingia darasani Januari mwaka huu, aliarifiwa kuwa amepata ‘mume’ na anatakiwa kuanza maisha mapya ya ndoa.

Anaambiwa hayo na kuonyeshwa mwenza mtarajiwa na wakwe zake waki wameshafika nyumbani kwao, lakini hakuwa tayari na hakukubali.

Alisema ‘nooo’ na akaazima baiskeli na kukukimbilia ofisi ya mtendaji kata wa Pandagichiza, akitembea zaidi ya kilometa 10 kuifikia na kutoa taarifa kuwa baba yake badala ya kumsomesha kidato cha kwanza, amemwandalia mume na saa chache zijazo anamuoza.



Wasichana na wavulana wana haki ya kusoma, waendelezwe kielimu badala ya kuozwa udogoni. **PICHA: MTANDAO**

Ofisi ya Mtendaji ilitoa taarifa dawati la polisi ili kumkamata mtuhumiwa, lakini alitoroka kabla ya kutiwa pingu, ikiwa ndiko kuokoka kwake.

Ndizo athari za mila na desturi kandamizi mkoani Shinyanga, zisizowathamini watoto wa kike, kuwageuza vitega uchumi vya familia na kuwabagua katika elimu na pale wanapohitimu darasa la saba au wakipevuka, hutafutiwa waume na kuwaozwa ili familia zinufaike kwa mali au mifugo.

Nipashe ilipata taarifa za tukio la mwanafunzi huyo kuozwa na baba yake na kuzichapisha Machi 1 2022, makala ikiwa na kichwa cha habari “Baba kuuza mabinti wakimaliza la saba, anawaandalia wachumba”.

Habari hiyo ilichangia kumnusuru na ndoa ya utotoni, ikiwaamsha wadau mbalimbali na viongozi wa serikali kutoa maagizo ya kufuatiliwa wanafunzi wote ambao wamehitimu darasa la saba na kufaulu wafuatiliwe na ambao wameshaozeshwa waondolewe kwenye ndoa na wapelekwe shule.

John Myola ni Mkurugenzi wa Shirika la Agape ambalo linalea wasichana walioathirika na matukio ya mimba na ndoa za utotoni, anasema baada ya kupata taarifa ya mwanafunzi huyo kutaka kuozeshwa, walimsaidia na kumsomesha katika shule ya Sekondari ya Mwangulumbi iliyoko Chibe Manispaa ya Shinyanga.

Anasema shirika hilo limekuwa likiwasomesha watoto hao walioathirika na mimba na ndoa za utotoni tangu mwaka 2015 mpaka sasa na kwamba wameshasomesha wanafunzi 267, tisa wamehitimu vyuo vikuu, 22 bado wanaendelea na vyuo, wengine wakisoma kidato cha sita, tano na sekondari.

**SHULE RAHA**

Akizungumza na Nipashe iliyomtembelewa shuleni, binti huyo, anaeleza kufarijika sana kuwa darasani kidato cha kwanza na anaamini atatimiza ndoto zake za kuwa mwalimu na msaada kwa familia yake na waathirika wengine.

Anakumbushia kuwa siku alipotaka kuozwa na baba yake mzazi, alijisikia vibaya akikumbuka namna dada zake walivyoozwa wakiwa watoto, mateso na masumbuko wanayopitia, ugumu wa maisha na machozi kila wakati, ndipo alipogoma ili kwenda shule licha ya baba yake kung’ang’ania aolewe sababu alishachukua mahari ya ng’ombe 14.

“Baba yetu haishi nasi amem-

INAENDELEA UK.14

ELIMU
NA GWAMAKA
ALIPIPI

# ‘Uwezo Award’ tuzo inayopika wanafunzi kuwa wajasiriamali



Wanafunzi wa Sekondari ya Kibaha wakifurahia tuzo baada ya kukabidhiwa na Mtendaji Mkuu wa Karimjee Jivanjee Foundation, Careen Rowland. **PICHA: TUZO AWARD**

MOJA ya mikakati ya kumjenga mwanafunzi kimaisha kabla ya kumaliza elimu ni kumfundisha ujasiriamali kwa vitendo anapokuwa darasani ili akimaliza shule autumie badala ya kuwa tegemezi.

Mkakati huo unamwezesha mwanafunzi wa ngazi ya elimu ya msingi na sekondari kufanya shughuli za ujasiriamali wakati anapokuwa nyumbani akisubiri matokeo ya mitihani au nyakati za likizo ama akishamaliza shule.

Shirika lisilokuwa la kiserikali la Great Hope Foundation limekuwa likitekeleza mkakati huo kupitia mradi wa ‘Uwezo Award’ ambao umejikita katika kuwapa nafasi wanafunzi wa sekondari kujifunza ujasiriamali kwa vitendo wakiwa shuleni.

Mratibu wa Uwezo Award, Noelle Mahuvi, anabainisha kwamba mradi huo unaendeshwa kwa njia ya mashindano na kwamba wanafunzi hushindana kufanya miradi mbalimbali ya kijasiriamali na ya kibunifu, ambayo inaleta matokea chanya katika jamii inayowazunguka.

**VIGEZO MUHIMU**

Mahuvi anasema miradi hiyo inakuwa na vigezo vikubwa vitatu kwanza, kuwapa nafasi ya kujitambua na kutumia uwezo wao, ambao mara nyingi hauonekani kwa urahisi.

Pili, anasema miradi hiyo inapaswa kuwapa nafasi kupata ujuzi na mwisho kuleta mabadiliko chanya katika jamii inayowazunguka ndani na nje ya shule.

> “ Tangu mwaka 2016, hadi 2021, Uwezo Award imezifikia shule za msingi na sekondari zaidi ya 620 za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Anabainisha kwamba shirika linawapa wanafunzi muda maalumu wa kufanya miradi hiyo ambao ni takribani miezi sita na kila waliozingatia vigezo hupata tuzo katika madaraja matatu.

Anazitaja kuwa ni tunzo za dhahabu kwa miradi bora sana, ya fedha na shaba kwa miradi ya kawaida, hata hivyo zawadi hiyo haiendani na msaada ya kuongeza au kuendeleza mradi alioubuni.

**WANUFAIKA**

Mahuvi anasema tangu mradi uanze, umewafikia wanafunzi 12,000 kutoka shule mbalimbali ambao walishiriki katika Uwezo Award tangu 2016.

Mratibu huyo anasema tangu mwaka 2016, hadi 2021, Uwezo Award imezifikia shule za msingi na sekondari zaidi ya 620 za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Anasema kupitia miradi ya kijasiriamali ambayo pia imekuwa ikileta mabadiliko chanya kwa jamii za shule yao, wanafunzi wamefanya mambo mengi kuboresha mazingira ya shule yao.

Akitolea mfano, Mahuvi anasema mwaka huu Sekondari ya Airwing iliyoko Dar es Salaam , wamekuwa washindi wanne wakipata tuzo kutokana na mradi wao wa kufuga panya na samaki wanaotumiwa kwenye maabara na wanafunzi wanaosaoma bailojia.

Kazi yao iliiwezesha shule hiyo kununua wanyama hao wanaotumiwa za maabara kwa bei nafuu, kuliko ambavyo shule imekuwa ikiwanunua sehemu nyingine kwa bei kubwa.

“Pia wanafunzi wa Kibaha, kupita mradi wao wa kijasiriamali waliouita, “Eagles Eye”, walikarabati madawati 40 ya shule yao, kuanzisha kilimo cha mboga za majani na kuwalisha wanafunzi na ziada kuuzwa kwa jamii inayo jirani na shule.

Anasema pamoja na shule kunufaika na miradi hiyo, wanafunzi wanaondoka na ujuzi ambao, unawasaidia kufanya ujasiriamali wanapokuwa nyumbani na popote pale.

Mratibu huyo anasema Shirika la Great Hope Foundation, baada ya kuona jitihada za wanafunzi wanazofanya katika miradi yao ya kijasiriamali, linarekodi miradi hii kwa kutengeneza makala fupi na kuziweka kwenye mitandao yao.

Anasema kwa mwaka 2021, Shirika la Great Hope Foundation, lilianzisha uwezo bonanza siku ambayo wanafunzi hushindana kuonyesha vipaji katika maeneo mbalimbali kama kuimba, kucheza, kuchora, kughani mashairi na kuruka sarakasi.

“Siku hii ilianzishwa kutokana na maombi ya wanafunzi ambao walitaka wawe na siku maalumu kuonyesha vipaji kwa sababu muda ambao tulikuwa tunawatengea, katika tamasha la kutoa tuzo, ulikuwa hautoshi,” anasema Mahuvi.

“Kwa mwaka jana, vikundi vilivyoshiriki ni pamoja na vya ngoma za utamaduni, kucheza, kuimba, kuchora, maigizo na sarakasi”.

Anasema Sekondari ya Hananasif, ilikuwa kinara wa kucheza wakati Sekondari ya Makongo ilishika nafasi tatu ambazo ni kuchora, ngoma za utamaduni na kuimba.

Mahuvi anasema mshindi wa maigizo ilikuwa ni Shule ya Sekondari Barabara ya Mwinyi na kwamba mwaka huu, uwezo bonanza inatarajiwa kufanyika Septemba.

**MIKAKATI MIPYA**

Mahuvi anasema kwa mwaka huu, Great Hope Foundation imeongeza miradi, ambayo wanafunzi wanatakiwa kuifanya kama sehemu ya mashindano.

Anasema wanafunzi wanapaswa kufanya miradi ambayo inaweza kuleta matokeo yenye kudumu kwa muda mrefu, kwa zaidi ya miaka miwili hadi mitano.

“Tumeiita Uwezo wards chain projects, pia shirika limehamasisha wanafunzi kufungua klabu za uwezo shuleni, ili waweze kufanya miradi endelevu inayotoa fursa kujifunza na kupata ujuzi mwingi katika maeneo mbalimbali utakaowasaidia kupambana na ukosefu wa ajira wakitoka shuleni,” anasema Mahuvi.

Anaongeza kuwa mwisho wa Oktoba wanatarajia kuwa na tamasha la tuzo za uwezo ambapo shule zilizofanya vizuri katika miradi ya uwezo award zitapewa tuzo.

**MIPANGO YA BAADAYE**

Mahuvi anasema kitu kikubwa ambacho wamejifunza katika miaka ya hivi karibuni ni kuwa wanafunzi na vijana wana uhitaji mkubwa wa majukwaa yanayowasaidia kukuza ujuzi na kuwapa maarifa endelevu ili waweze kuwa na manufaa katika soko la ajira.

Anasema Great Hope Foundation inakusudia kuainisha miradi mingine bunifu, itakayosaidia kuwapa nyezo vijana wanaopitia katika uwezo award na kwamba wanaandaa mradi wa ‘uwezo forum,’ wa kutoa mafunzo kwa vijana wanaoanzisha biashara au wenye mawazo ya biashara wanaotokana na ‘uwezo award.’

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Kilio taulo za kike wadau watamani 'pedi za kudumu'

MABINTI wa leo ni wazazi na walezi wa kesho, hao ndiyo watakaozaa na kulea nguvu kazi na kuijenga Tanzania, hivyo bila wasichana hawa kuwa na afya bora ni dhahiri hawatakuwa na watoto wenye siha ambalo ni taifa imara.

Aidha, afya bora ya uzazi huanza na hedhi salaama , ndiyo maana kilele cha maadhimisho ya hedhi salama kilichohitimishwa Mei 28, mkoani Kigoma, kikiwa na kaulimbiu 'hedhi ni tunu na msingi wa afya, dhamiria kuwekeza katika nyanja zote', kinaweka mkazo wa kulinda uzazi kwa wasichana.

Kabla ya kufikia kilele hicho, wadau wa hedhi salama wanafanyika shughuli mbalimbali ikiwamo kugawa taulo za kike kwa wanafunzi kusaidia kupunguza tatizo la kukosa shule na kupunguza kutohudhuria masomo wakati wa hedhi.

Hatua hiyo inachukuliwa kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wanafunzi wanakosa masomo kwa siku kadhaa kutokana na kukosa vifaa vya kujisitiri wakiwa kwenye siku hizo.

Sababu hiyo inawalazimisha kubaki nyumbani kwa siku hizo kila mwezi jambo linalowarudisha nyuma kimasomo.

Kutokana na mazingira hayo, wadau wanashauri serikali kuruhusu uzalishaji wa taulo za kike zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja ili wanafunzi wengi zaidi na wanaotoka kwenye familia zenye kipato kidogo ziweze kufaidika.

Mmoja wa wadau hao ni Mkurugenzi wa asasi ya kiraia ya Victoria Foundation, Victoria Kamata, anayeshauri serikali kumaliza mjadala wa kuzalishwa na kutumika pedi zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja.

Pedi hizo ni muafaka maana zinaweza kutumiwa kisha kufulia na kunyooshwa na kuendelea kutumika zaidi, ya mara moja hivyo suala kupata ufumbuzi na idhini kupatikana ni muhimu, anasema Kamata.

Anaongeza kuwa suala hilo linagusa elimu, maisha na afya za mabinti hao hasa wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini, na kwamba wanalazimika kuokoteza vitambaa visivyo rasmi na kuvitumia jambo linalohatarisha afya ya uzazi kwa watoto hao.

Anakumbusha kuwa serikali ikiruhusu matumizi ya taulo hizo itatoa uhakika wa hedhi salama kwa wanafunzi wanaoishi vijijini, ambako familia za walio wengi hazina uwezo wa kumudu kuzinunua.

"Familia nyingi za wanafunzi wa vijijini zinataabika kununua taulo hizo kila mara na kusababisha baadhi ya wanafunzi kutokwenda shule wanapokuwa katika hedhi na wengine hulazimika kuacha masomo," anasema.

Hayo ni maoni yake wakati akizungumza na gazeti hilo baada ya kukabidhi taulo 1, 878 kwa wanafunzi 626 wa shule nne za sekondari za Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi.

Sekondari hizo zilizonufaika na msaada huo ni Marry Majaliwa iliyopo katika kata ya Nandagala, Hawa Mchopa, Mnacho Sekondari na Lucas Maria za kata ya Mnacho.

Kamata anasema, licha ya kutokuwa na takwimu sahihi za idadi ya wanafunzi wanaokatisha masomo kwa kukosa taulo, anaamini changamoto ni kubwa huku akiomba kuharakishwa kuruhusu utumiaji wa taulo zaidi ya mara moja.

"Wenye mamlaka waruhusu taulo zinazoweza kutumika zaidi ya mara moja ili kuleta uhakika kwa mabinti zetu popote pale walipo ili kuepusha kukatisha msomo kwa baadhi ya siku, kwani hali hiyo si nzuri kielimu," anasema.

Anasema taasisi yake imetoa taulo hizo kwa ufadhili wa Benki ya NMB kupitia mradi wa kitaifa wa 'Binti Ng'ara Fikia Malengo', ambapo kabla ya kwenda Ruangwa, ilianzaa kugawa taulo hizo katika shule za mkoani Simiyu.

"Victoria Foundation imedhamiria kusaidia mabinti, lakini kuwapunguzia wazazi na walezi mzigo, hivyo tunaweza tusifikie malengo iwapo uamuzi wa kutumia taulo endelevu hautaruhusiwa," anasema.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Victoria Foundation, Vicky Kamata, akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Lucas Maria, kabla ya kugawa taulo za kike. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

> Victoria Foundation imedhamiria kusaidia mabinti, lakini kuwapunguzia wazazi na walezi mzigo, hivyo tunaweza tusifikie malengo iwapo uamuzi wa kutumia taulo endelevu hautaruhusiwa.

### WAPEWA SEMINA

Mratibu wa Programu wa mradi huo, Steven Mruma, anasema kabla ya kugawa taulo hizo, taasisi yao ilipata fursa ya kuendesha semina kwa wanafunzi wa shule hizo ambapo Zamaradi Mketema alitoa mada kuhusu wasichana kujitambua ili wasikwame katika kufanya uamuzi na kuchukua hatua sahihi kwa wakati hasa wanapokutana na wanaume wadanganyifu.

Anafafanua kuwa katika semina hiyo anawahimiza wanafunzi mabinti kutambua familia zao zina matumaini makubwa juu yao hasa katika siku zijazo, hivyo njia pekee ya kufikia malengo ni kujitambua na kuchukua hatua sahihi.

"Kwa upande wa wanafunzi wa kiume, mtoa mada alikuwa Emmanuel Mathias au 'MC Pilipili', ambaye aliwapitisha katika umuhimu wa kutumia kikamilifu mitandao ya kijamii kwa faida ya masomo yao," anasema Mruma.

Mdau mwingine ni Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa, Hassan Ngoma, anawapongeza wadau wote kwa kubuni mradi huo na hasa kwa kuchagua Wilaya ya Ruangwa na kusaidia wanafunzi wake.

Anasema Victoria Foundation ni wadau wanaofaa kuigwa na mashirika mengine katika jitihada za kuwasaidia mabinti walioko shuleni kupambana na changamoto zinazowarudisha nyuma.

Ngoma anawashauri wazazi na walezi wenye wanafunzi wa kike kuanza kuweka akiba ya shilingi 100 kila siku ili kuwanunulia taulo za kike badala ya kununua vitenge vipya kila mwisho wa mwezi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, anasema anatamani kuiona tena Victoria Foundation ikirudi Ruangwa kusaidia mabinti hao na wengine baada ya miezi mitatu ijayo.

### ELIMU KWANZA

Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, anasema, utoaji wa taulo hizo kwa wanafunzi wa kike ni moja ya kurudisha faida wanayopata kutoka kwa jamii na kwamba elimu ndiyo kipaumbele namba moja cha benki hiyo.

Faudhia Matandi, mwanafunzi wa kidato cha pili katika Sekondari ya Lucas Maria, ananufaika na taulo hizo anasema amefarijika kupata msaada huo na kusema utapunguza siku ambazo mabinti wanashindwa kufika shuleni.

"Wasichana tunakosa kuhudhuria masomo kwa wastani wa siku tano hadi saba kwa mwezi sawa na siku 36 hadi 87 kwa mwaka ambapo wakati tunakosa masomo, wenzetu wa kiume wanaendelea kusoma na mitihani inapokuja hakuna anayetuonea huruma," anasema Faudhia.

# Manusura ndoa utotoni asherehekea

INATOKA UK.11

wacha mama na ameshaoa mwanamke mwingine huko Tabora, anafuatilia akisikia tumehitimu darasa la saba anakuja kutuozesha na kuondoka na mifugo kwenda nayo Tabora huku mama akibaki bila kitu nikaona kuna haja ya kukataa ukatili huo, sikuona sababu ya kuolewa, hakuna faida zaidi ya kwenda kunyanyasika kama yalivyomkuta dada yangu," anasema mwanafunzi huyo jasiri.

Anaishukuru Nipashe kwa kupigania ndoto zake akisema: "Leo mmekuja hapa shuleni kuona maendeleo yangu, kwa kweli naendelea na masomo ninapata mahitaji yote ya shule, nafuraha sana sababu na kwenda kutimiza ndoto zangu za kuwa mwalimu na kuikomboa jamii yangu."

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), anasema anafuraha kumuona mwanawe akiendelea na masomo na kueleza kuwa atakuja kuwa msaada kwenye familia yao, sababu dada yake ambaye alikuwa tegemeo yeye aliozeshwa akaachishwa masomo.

"Sina uwezo kama maisha yetu ni magumu na hata fedha za kumsomesha sina, nashukuru Shirika la Agape kumsomesha mwanangu na kuishi naye huko mjini, sababu angeendelea kukaa hapa kijijini baba yake lazima angerudi na kumwozesha kwa nguvu, lakini sasa nina imani atatimiza ndoto zake," anasema mama mzazi.

### ATHARI KIMASOMO

Boniphace Charles ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Mwangulumbi, anasema hali ya mwanafunzi huyo kitaaluma ni wastani sababu akizieleza kuwa ni tukio hilo la kutaka kuozeshwa kwa nguvu na kumwathiri kisaikolojia.

"Limemwathiri na wakati mwingine akilikumbuka huanza kulia lakini naamini atakaa sawa na kufanya vizuri zaidi sababu ana akili na juhudi kubwa," anasema Charles.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omari, anasema walichokifanya kwa mwanafunzi huyo ni kumwekea ulinzi, kwa kumfungulia baba yake kesi polisi, licha ya kukimbia na hajulikani alipo, ili asimfuate tena na kumbughudi.

Asha anasema tatizo ambalo limekuwa likichangia matukio ya mimba na ndoa za utotoni kuendelea wilayani humo na Mkoa wa Shinyanga, ni jamii kuendekeza mila na desturi kandamizi za kutothamini mabinti wengi wakiwaozesha ili wapate mifugo.

"Takwimu za mimba za wanafunzi na ndoa za utotoni wilayani hapa tangu mwaka 2020 hadi Aprili 2022, zinaeleza kuwa wanafunzi 100 wameshapewa ujauzito, huku wanne wakiozeshwa ndoa za utotoni, na watatu wameondolewa kwenye ndoa na wanaendelea na masomo," anaongeza.

Anasema halmashauri hiyo inashirikiana na Jeshi la Polisi katika mapambano ya kutokomeza ndoa za utotoni, na hata kufikia hatua ya kuvamia sherehe za ndoa na kuzitibua.

"Uvamizi wa shughuli za ndoa na kuwakamata watuhumiwa, umesaidia kupunguza matukio ya ndoa za utotoni, ambapo awali ndani ya mwaka mmoja wanafunzi 20 walikuwa wakiolewa lakini sasa ndoa hizi zimepungua na kutokea ndoa nne kwa mwaka," anasema Asha.

### BABA HAJANASWA

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, anakiri baba mzazi wa mwanafunzi huyo amefunguliwa jalada lenye kumbukumbu RB SHY/RB/ 231/ 2022 na anaendelea kutafutwa.

Anaongeza kuwa alikimbia watuhumiwa wengine 16 wa kesi kama hizo ambao nao hawajulikani walipo.

"Tunapowakamata watuhumiwa hawa huachiwa kwa dhamana, lakini wakirudi tu huko uraiani hukimbia na hata kuhama mji na kwenda kusikojulikana, lakini tutaendelea kuwatafuta.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, anasema tatizo la mila na desturi limekuwa kikwazo cha kutokomeza mimba na ndoa za utotoni mkoani humo.

Anawataka maofisa maendeleo na ustawi wa jamii wa halmashauri zote mkoani humo, pamoja na mashirikia yasiyo ya kiserikali kuendelea kutoa elimu ya kupinga mila hizo kandamizi za kuozesha wanafunzi zinazozorotesha maendeleo.

Anasema jamii haina uelewa wa athari za kuozesha wanafunzi ndoa za utotoni, lakini wakipata elimu hiyo kikamilifu pamoja na kuijua sheria ya mtoto ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019, na sera ya elimu ya mwaka 2008, hawatafanya vitendo hivyo.

### MUHALI MITAANI

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mkoa wa Shinyanga, Mary Mrio, anabainisha tatizo lingine ambalo linasababisha mimba na ndoa za utotoni kuendelea mkoani humo, ni wazazi, walezi.

Anasema kutokana na tamaa ya fedha au kuoneana aibu wahusika wanazimaliza wenyewe kwa makubaliano wanayofikia na kusababisha kesi kufutwa sababu ya kukosa ushahidi.

"Kesi inafunguliwa mahakamani wakati ikiendelea kusikilizwa na kupangwa tarehe, siku ya kusikilizwa, mwanafunzi anamkana mtuhumiwa, na ukiwabana zaidi wanahama mkoa na kwenda kuishi kwingine mwishoni inabidi umwachie huru mtuhumiwa na kuifunga kesi," anasema Mary.

"Washtakiwa wangekuwa wakifungwa jela, sidhani kama mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga zingekuwapo tena..." anaongeza.

Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Shinyanga, Ushindi Swalo, anasema mahakama hiyo imeanzisha utaratibu wa kusikiliza mashauri ya kesi za watoto, kwa kuitenga Ijumaa siku maalumu ya kusikiliza kesi hizo ndani ya muda mfupi na kutolewa hukumu haraka kulingana na ushahidi.

Mratibu wa mpango mkakati wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto mkoani Shinyanga Tedson Ngwale, anasema katika kukabiliana na tatizo la ndoa za utotoni mkoani humo, wameanza mchakato wa kutunga sheria ndogo ambayo itadhibiti ufungishaji wa ndoa za utotoni.

Anasema vipengele vya sheria hiyo vitakuwa na kujaza fomu za ndoa, pamoja na kufanya tathmini ya ndoa kabla ya kufungwa, ili kujiridhisha kama ndoa hiyo haozeshwi mtoto pamoja na kuangalia miaka yake katika vyeti vya kuzaliwa, hali ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kutokomeza ndoa za utotoni mkoani Shinyanga.

"Fomu za ndoa zitakuwa zikipatikana kwenye ofisi za watendaji wa vijiji na sheria hii ndiyo itakuwa mwarobaini wa kutokomeza ndoa za utotoni hapa," anasema Ngwale.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anakemea vitendo vya wazazi kugeuza watoto vitega uchumi na kuwaozesha ndoa za utotoni, na kuagiza watendaji wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji, maofisa elimu na maendeleo ya jamii, kufuatilia wanafunzi wote ambao wameacha masomo ili kujua wako wapi na kama wameshaolewa wahusika wachukuliwe hatua.

## WANENAVYO MALENGA

### WIVU USIMUONEE

Ukiachana na mtu, wivu usimuonee,
Aondoke roho kwatu, mate usimtemee,
Kwako alifanya kitu, kule usiyasemee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Aagwe vizuri mtu, kwingine aendelee,
Kusiwe maneno kutu, akenda umkemee,
Tambua kesho si yetu, anaweza arejee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Pengine huyo ni mke, umetaka apotee,
Mfungashe aondoke, tena usimmezee,
Mapya acha aandike, na usimsogelee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Kenda huko aolewe, eti ameenda chee,
Ni vipi aingiliwe, na fujo uzichochee?
Wakati wewe mwenyewe, limwambia apotee?
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Mume ulimwita bwege, na kwako asisogee,
Eti ni mbeba zege, hawezi akupepee,
Wapenda kupanda ndege, ubaki uchekelee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Mwanaume kainuka, sasa mali kwake ndee,
Jimama unashituka, ukitaka asogee,
Ninakwambia futika, na mawazo ya kizee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Agana na mtu wako, maisha yaendelee,
Huhusiki aendako, acha usiongelee,
Kwako amekuwa mwisho, wala usimzomee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Dunia duara hii, acha tuiongelee,
Ulowaambia zii, huko wasiogelee,
Wako juu hufikii, makali uyapokee,
Shukuru mlipofika, shika hansini zako.

Nawe unayeondoka, hiyo kambi usinyee,
Pengine huko kifika, kwamba utokelezee,
Yale utayoyakuta, waweze sichekelee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

Aondoka baibai, baraka azipokee,
Pengine kwako hafai, wengine wampokee,
Unaweza pata chai, na kwake akupokee,
Shukuru mlipofika, shika hamsini zako.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### KUONGOZA UPOTOFU

Acha uongozi huko, bora uhamie huku,
Uendako huko siko, utulivu uko huku,
Hakueleweki huko, wengi wahamia huku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Ni genge majambazi, wewe umeshika luku,
Waambiwa siyo kazi, wazidi nyoa kiduku,
Wanafyekwa wote wezi, wazidi ufukunyuku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Mkuu wa Panya Rodi, wasumbua kila siku,
Kazi haina akidi, sawa mboga chukuchuku,
Mausia wakaidi, waona hiyo ni daku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Meponea chupuchupu, kunyolewa kama kuku,
Wazidi mwaga upupu, pamoja na kukushuku,
Waiba wajaza kapu, watu watoka mkuku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Uitwe ni kiongozi, kwa hao mazumbukuku?
Kweli hiyo kwako kazi, kuwangawanga usiku?
Si ungefanya palizi, chakula chako cha siku?
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Unasifika kwa rushwa, kila siku wala kuku,
Hata kama unatishwa, kwako haipiti siku,
Ni kama vile wawashwa, unavyokusanya buku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Kweli unaipofua, kwa wako ufukunyuku,
Uongo waona jua, mchana wawa usiku,
Mambo unayapindua, kwa mwendo wa tukutuku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

Mwisho wako wewe giza, hakuna wa kukutunuku,
Hapana kama wapendeza, kule shida kila siku,
Tajiri Lazaro waza, liwe ni Neno la siku,
Kuongoza upotofu, ni maangamizi yako.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# Watakiwa kutumia teknolojia ya kisasa kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Mtendaji wa Shirika la Agriculture Seeds Production Association (DASPA), Aithan Chaula, amewataka wakulima kutumia teknolojia za kisasa ili kuongeza uzalishaji wenye tija ikiwamo kupunguza gharama wakati wa msimu wa kilimo.

Chaula, alisema wakulima wakitumia teknolojia ya kisasa kupalilia, kupanda hadi msimu wa mavuno kwa kutumia zana za kisasa kutawasaidia kupunguza gharama na kutawaongezea mavuno.

Alisema wakitumia mashine ya kupandia ikiwamo kutumia teknolojia ya kupalilia anaamini wakulima watafanya kilimo chenye tija ambacho kitawapatia mavuno mengi.

Alisema kuwa mwaka jana gharama za kupalilia ekari moja zilikuwa Sh.70,000 hadi 100,000 ambayo wakulima wengi walishindwa kuimudu, ndiyo maana anasisitiza wakulima wajiunge pamoja kutumia teknolojia ya kisasa kwa ajili ya kuendesha kilimo.

"Hapa shambani kwangu chupa ya kuua magugu nilinunua kwa Sh. 18,000 na ilitosha eneo la ekari moja hivyo nilipunguza sana gharama, wakulima wajifunze hii teknolojia kwani ni rahisi na inaokoa sana muda," alisema Chaula.

Naye Mkulima Nassoro Mazengo, aliiomba serikali kusambaza kila eneo teknolojia ya mashine za kupandia na kuua magugu mashambani ili kusaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kufanya kilimo kiwe na tija.

Mazengo alisema ni vyema serikali ikabeba dhamana ya kuhakikisha teknolojia za kisasa ikiwemo mashine za kupandia na matumizi ya madawa ya kuua magugu zinawafikia wakulima jambo ambalo litasaidia kuinua kilimo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kutoka kituo cha Makutupora, Dk. Cornel Massawe, aliwataka vijana kuwa na kiu ya kujifunza teknolojia za kisasa na kuachana na kilimo cha mazoea ambacho kimekuwa kikitumia nguvu kubwa tija kidogo.

Dk. Massawe alisema kuwa kundi kubwa lililojitokeza kwenye maadhimisho ya Siku ya Mkulima ni Vijana ambao wana kiu ya kujifunza kuwapa manufaa katika kilimo.

"Kuna kitu ambacho wamejifunza na bado kuna udadisi wa kutumia teknolojia na kuileta kwa wakulima hapa wameona teknolojia mpya kwa macho yao tusifanye kilimo cha mazoea, tija ijengwe ndani ya malengo," alisema Dk. Massawe.

Mtafiti Mwandamizi kutoka Shirika la Utafiti wa Mazao yanayomea Mtandao Kame (ICRISAT), Wills Munthali, kutoka nchini Malawi alisema awali lilifanyika dodoso na kulikuwa na changamoto kama ukame uliokithiri, mafuriko na uhaba wa mbegu bora.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo TARI Hombolo na wakulima wa wilaya ya Kiteto waweze kuona mbegu zinazofaa katika maeneo yao.

Alisema kumekuwa na utaratibu wa kuwapatia mbegu wakulima ambapo kila mmoja alipewa kilo tatu za mbegu anatakiwa kurudisha mara mbili zaidi ili wakulima wapate.

# Marufuku kelele katika nyumba za ibada, baa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amepiga marufuku mahubiri ya sauti za juu katika makanisa wakati wa usiku pamoja na kelele ya muziki kwenye baa zilizo kwenye makazi ya watu.

Mtaka, alipiga marufuku hiyo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Kisasa, kuhusu kuimarishwa ulinzi na usalama kutokana na kuripotiwa kwa matukio mbalimbali ya uhalifu katika eneo hilo.

Alisema, Idara ya Mazingira Jiji la Dodoma inapaswa kuanza kufanya ukaguzi katika nyumba za ibada ambazo zimekuwa zikifanya mahubiri kwa sauti za juu na kukwaza watu wengine.

"Ni marufuku kuanzia leo (juzi) mahubiri ya makelele katika nyumba za ibada, kama unapiga mapambio piga ndani ya kanisa lako isiwe kero kwa watu wengine kuwakwaza na mahubiri yako pia wanaopiga muziki kwa sauti za juu kwenye baa zilizo katika makazi ya watu ni marufuku kuanzia leo," alisema Mtaka.

Mtaka, alisema jiji linapaswa kutumia sheria zake kuwawajibisha watu wote watakao kaidi agizo hilo kwa kuwatoza faini kwa mujibu wa sheria ndogo ndogo.

"Hii ndiyo fursa ya jiji kujipatia fedha ili kujenga miundombinu mingine binadamu bila kupigwa adhabu hawezi kubadilika hivyo kamateni hawa wote piga faini tupate fedha za kujenga ofisi za mitaa," alisema Mtaka.

Kadhalika, alisema mkoa utaandaa kikao na viongozi wote wa makanisa ili kuona namna ya kujadiliana kuhusu suala hilo.

"Tunaandaa kikao kati yetu na viongozi wa dini mahubiri kwa sauti kali na miziki ya makelele ya juu usiku hapana na hii ianze kutekelezwa leo," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema agizo hilo watayafanyia kazi kupitia wataalamu wake wa mazingira.

Mafuru alisema Jiji la Dodoma linakua kwa kasi kutokana na ujio wa makao makuu na maendeleo yanakuja na changamoto mbalimbali ambazo wanapaswa kuzifanyia kazi.

"Hii ni kutokana na serikali yetu kuleta makao makuu kila mtu hivi sasa anaiangalia Dodoma na watu wengi wanakuja na mambo mbalimbali ambayo wanaona yatawapatia kipato wakati mwingine wanavunja sheria," alisema Mafuru.



Mkuu wa Miamala wa Benki ya NMB Makao Makuu, Linda Teggisa (kulia), akiwasilisha mada kuhusu huduma zinazotolewa na NMB kwenye kongamano la kitaifa la wahandisi na makandarasi wa miundombinu la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake katika kuimarisha makandarasi wa ndani, jijini Dodoma juzi. NMB walidhamini kongamano hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PBZ yatoa msaada vifaa tiba wodi ya watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imetoa msaada wa vifaa tiba na vyakula kwa wodi ya watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali kuboresha huduma za afya nchini.

Meneja wa Benki hiyo tawi la Dodoma, Mohamed Masoud, akikabidhi msaada huo alisema kuwa lengo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha huduma za afya nchini.

"Leo hii tumekabidhi vifaa tiba katika hospitali yetu ya rufani ya Mkoa wa Dodoma, ikiwa ni kuonyesha ushirikiano wetu kwa jamii na kuthamini kile ambacho serikali yetu inakifanya kuboresha seka hii muhimu ya afya nchini," alisema Masoud.

Alisema, vifaa walivyokabidhi ni pamoja kiti mwendo kwa ajili ya wagonjwa wasioweza kutembea, mashuka na maziwa kwa ajii ya watoto ambao wazazi wao hawatoi maziwa ya kutosha vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 3.5.

"Leo tumekuja, lakini hii haitakuwa mwisho tutaendelea kuja na kuona mahitaji yaliyopo hapa ili kuwahudumia watu mbalimbali wenye uhitaji," alisema.

Muuguzi Mfawidhi wa hospitali hiyo, Stanely Mahundo, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo ambao umekuja wakati mwafaka na utatatua baadhi ya changamoto walizokuwa wakikabiliana nazo.

Alisema lengo la serikali ni kuboresha miundombinu ya afya hivyo wadau wakishiriki kusaidia kutatua baadhi ya kero wataiwezesha kupiga hatua.

"Wito wangu ni taasisi zingine kuiga mfano wa benki hii ili kuja kuungana na serikali yao katika kuboresha huduma za afya nchini," alisema.

Alisema anaishukuru serikali kwa kuboresha huduma mbalimbali katika hospitali hiyo na hivi sasa wanatoa huduma za kibingwa zaidi ya 20.

"Na katika mwezi mmoja ujao tunakwenda kuzindua wodi ya ICU kubwa ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa zaidi ya 60, pia kwa ajili ya watoto na wagonjwa wengine, pia huduma za upasuaji tumeziboresha sana zinapatika na za uhakika katika hospitali yetu," alisema Mahundo.





# Mataifa 7 kuhudhuria Nanenane Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAANDALIZI ya Maonyesho ya Wakulima Nanenane kitaifa, yameanza kupamba moto mkoani Mbeya na wajasiriamali kutoka mataifa saba wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wanatarajiwa kushiriki.

Maandalizi ya maonyesho hayo yamegawanyika katika makundi matatu, ya kitaifa, ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kimkoa.

Akizungumza kwenye kikao cha maandalizi cha Mkoa wa Mbeya kilichowahusisha wadau mbalimbali wa mkoa huo, Mkuu wa mkoa huo, Juma Homera alisema, maonyesho ya mwaka huu yana uzito kuliko ya miaka yote.

Alisema wanatarajia kualika waonyeshaji kutoka mikoa mbalimbali ya nchi jirani ikiwamo Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Malawi na Msumbiji.

Aliitaka sekretarieti ya maandalizi ya maonyesho hayo kuendelea kuboresha miundombinu ya viwanja vya John Mwakangale, yatakapofanyika maonyesho hayo na kwamba miundombinu hiyo inatakiwa iwe imekamilika kabla ya Julai 15.

Aidha, alizitaka halmashauri zote za mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambazo zinadaiwa malipo mbalimbali zikiwamo ankra za maji ili vipando viendelee kumwagiliwa kwa ajili ya maonyesho hayo.

"Sekretarieti ya maandalizi hakikisheni mnatafuta kampuni zenye mitambo ili zitusaidie mitambo ya kusafishia barabara zetu humu ndani sisi tutachangia mafuta," alisema Homera.

Mwenyekiti wa Sekretarieti ya maandalizi ya maonyesho hayo, Said Madito, alisema walifanya tathmini ya uchakavu wa miundombinu ya barabara za uwanja huo na kubaini kuwa gharama ni zaidi ya Sh. milioni 190.

Alisema gharama hizo zinatakiwa kubebwa na Kamati ya maandalizi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kuahidi kikao cha pili cha kanda kinachotarajiwa kufanyika Juni 9, mwaka huu, kitajadili na kupitisha bajeti hiyo.

Aidha, alisema kila halmashauri inatakiwa kugharamia ukarabati wa banda lake ili kuyaweka mazingira katika hali nzuri huku akisisitiza wananchi kuendelea kuhamasishwa ili wajitokeze kwenye maonyesho hayo.

"Kwa kuwa maonyesho haya yanafanyika kitaifa hapa mkoani kwetu, tunatarajia maeneo yote ambayo yalikuwa hayatumiki yatumike, tutasawazisha maeneo yote na kutengeneza barabara za mitaa," alisema Madito.

Baadhi ya wadau walioshiriki kikao hicho cha maandalizi, walishauri barabara za mitaa za uwanja huo ziwekwe vizuri na kuwekewa majina ya kila mtaa kama ambavyo imefanyika kwenye zoezi la anwani za makazi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba, alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni iliyofanya vizuri kwenye zoezi hilo na likitumika kwenye uwanja huo litasaidifu kilichoko mitaani.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Madini ya OreCorp Tanzania Ltd, wakifanya usafi wa mazingira katika kijiji cha Ngoma, wilayani Sengerema, mkoani Mwanza ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafugaji waomba muda uvalishaji hereni mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wilayani Chunya mkoani hapa, wameiomba serikali kuongeza muda wa utambuzi na uvalishaji hereni mifugo kutokana na zoezi hilo kuchelewa kuanza wilayani humo na kuhisi watashindwa kukamilisha.

Kazi hiyo inatarajiwa kufikia tamati Agosti 31, mwaka huu, hata hivyo, wafugaji wa wilaya hiyo wanasema mpaka sasa bado haijaanza na wilaya yao ni miongoni mwa maeneo yenye idadi kubwa ya mifugo katika mkoa huo.

Walitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki ziara ya Mwenyekiti wa chama cha wafugaji nchini, wataalamu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na wataalamu kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI).

Ziara ya wataalamu hao ilikuwa na lengo la kuwahamasisha wafugaji kushiriki zoezi hilo ili lifanyike kwa ufanisi na kufikia malengo ya serikali ya kutambua mifugo yote kwa ajili ya mipango mingine ya maendeleo katika sekta hiyo.

Mmoja wa wafugaji hao, Mtheo Shaban, alisema zoezi hilo ni zuri na ni mfumo wa kisasa unaotumika kutambua mifugo, lakini kwenye eneo lao wamechelewa kuanza na hawawezi kulikamilisha ndani ya miezi iliyobakia.

Aliomba waongezewe muda na ikiwezekana mwezi mmoja ili kukamilisha zoezi hilo na kwamba ikitokea zoezi hilo halijakamilika kwa ufanisi serikali itakuwa haijafikia malengo tarajiwa.

Vilevile alisema zoezi hilo litahusisha fedha na wafugaji wanatakiwa wapewe muda wa kujiandaa kifedha kwa ajili ya kutekeleza.

Katibu wa Chama cha Wafugaji wilayani Chunya, James Kidayi, alisema kwa sasa hawana takwimu sahihi za mifugo katika wilaya hiyo kutokana na mifugo mingi kutotambuliwa.

Alisema utambuzi wa mifugo utasaidia pia kuwa na takwimu sahihi wilayani humo jambo ambalo alisema litasaidia pia kuboresha huduma zao katika eneo hilo ikiwamo kutenga maeneo yao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Taifa, Jeremiah Wambura, aliwataka viongozi wa wafugaji kuendelea kuwahamasisha wananchi kutekeleza kazi hiyo badala ya kuanza kulalamika.

Alisema wafugaji wanatakiwa waendelee kusajili mifugo yao ili ikifika muda uliopangwa na serikali waanze kuomba kuongezewa muda.

Alisema serikali haiwezi kuanza kuongeza muda wakati kazi haijaanza na kuwataka wafugaji kuendelea kutekeleza kwa mujibu wa taratibu.

"Mkisajili mifugo 100,000 mpaka kufika mwisho na mingine ikawa imebaki hapo ndipo tunaweza tukawa na nafasi ya kuiomba serikali kuwaongezea muda wa kumalizia iliyobakia," alisema Wambura.

Mratibu wa Sekta ya Mifugo kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dk. Bertha Gugange, aliwataka wadau wote kushirikiana na wataalamu kutekeleza zoezi hilo ili lifanikiwe vizuri.

Ofisa Mifugo Mkoa wa Mbeya, Dk. Samora Mshang'a, alisema zoezi hilo linakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanalifanya lisifikie malengo kwa wakati mpaka sasa na kuomba ushirikiano wa wadau mbalimbali kulikamilisha ikiwamo kuhamasisha wafugaji.

# Wachimbaji wadogo madini watahadharishwa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, imewatahadharisha wachimbaji wadogo wa madini wilayani humo kuacha tabia ya kuchimba kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara ikisisitiza kuwa itawachukulia hatua kali za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliyasema juzi wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani ambayo kimkoa yalifanyikia wilayani humo na kushirikisha wadau mbalimbali wa mazingira.

Alisema wachimbaji hao wamekuwa wakiharibu miundombinu ya barabara kwa kuchimba madini kwenye maeneo ya hifadhi za barabara na wamekuwa wakichimba na kuacha mashimo kwenye maeneo hayo.

"Kuanzia leo ukikutwa unachimba madini kwenye maeneo ya hifadhi za barabara, tutakuchukulia hatua kali za kisheria, wewe hutakuwa tofauti na wahujumu uchumi hivyo ili kuepuka hilo ni vyema mkaacha kabisa," alisema Mayeka.

Vilevile, aliwataka kufanya shughuli hizo kwa kuzingatia sheria ikiwamo kuepuka kuchimba kwenye misitu ya hifadhi na vyanzo vya maji ili kulinda maeneo hayo.

Kwa upande wake mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, aliwataka wadau wote kushirikiana kulinda mazingira ikiwamo misitu ya asili ili kuepuka mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri dunia kwa sasa.

**Vilevile, aliwataka kufanya shughuli hizo kwa kuzingatia sheria ikiwamo kuepuka kuchimba kwenye misitu ya hifadhi na vyanzo vya maji ili kulinda maeneo hayo.**



## Wastaafu 441 vikosi ulinzi wakosa stahiki fomula ukokotoaji kukosewa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Maoud Muhammed, amesema kuwa jumla ya wastaafu 441 wa vikosi vya ulinzi walinyimwa kulipwa stahiki zao kutokana na kukosewa kwa fomula ya ukokotoaji ya malipo ya mafao hayo.

Alisema kati ya askari hao 419 tayari wameshalipwa tofauti ya stahiki za mafao yao baada ya kuhakikiwa kwa taarifa zao.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakililishi wa Jimbo la Pandani, Omar Fakih, aliyetaka kujua ni wastaafu wangapi waliopunjwa ambao wamelipwa na wangapi ambao hawajalipwa tofauti ya mafao yao ya kiinua mgongo na pensheni waliyopunjwa.

Waziri alisema jumla ya Sh. 3,761,568,251 zimetumika kulipa wastaafu hao na wastaafu 22 hawajalipwa tofauti ya stahiki za mafao yao kutokana na kutowasilisha taarifa za kibenki zikijumuisha namba ya akaunti na risiti ya malipo.

Alisema taarifa hizo zitatumika kuhakiki na kuepuka kufanya malipo mara mbili tofauti za malipo ya mafao hayo.

Alisema kuwa serikali iko tayari kutekeleza maamuzi ya Mahakama Kuu ya Zanzibar Novemba 22, 2016 ya kesi ya madai nambari 30 ya mwaka 2009 na jumla ya Sh. 239,580,123 zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa tofauti ya stahiki za mafao hayo.

# Upimaji UVIKO-19 wageni, wenyeji waendelea Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema kuwa bado inaendelea kutoa huduma ya kuwapima UVIKO-19 kwa wageni na wenyeji wanaosafiri nje ya nchi.

Hayo yalielezwa jana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Omar Fakih aliyehoji kuwa, pamoja na chanjo ya UVIKO-19 kutolewa bure Zanzibar, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu gharama za kufanyia vipimo vya UVIKO-19 kwa Zanzibar, kiasi cha kuchukuliwa kama anasa badala ya janga la kimataifa.

Naibu Waziri huyo alisema hivi sasa wanapima vipimo vya UVIKO-19 ambavyo vinavyopatikana ni vya aina tatu kulingana na mahitaji ya shirika la ndege au nchi ambayo msafiri anataka kwenda.

"Vipimo vyenyewe ni vya haraka (Ag. Rapid Test), "Rapid PCR Molecular Test na PCR ya kawaida...Mheshimiwa Spika, gharama ya vipimo hivyo ni kama ifuatavyo; PCR ya kawaida dola 80, "Rapid PCR Molecular Test dola 110 na "Antigen Rapid Test" dola 25," alisema.

Alisema kuwa ni wazi serikali imeathirika kwa kiasi kikubwa kimapato na kimatumizi kulikosababishwa na mahitaji ya moja kwa moja ya UVIKO-19.

Alisema kuwa uchumi wa nchi unategemea Sekta ya Utalii na uwapo wa janga la UVIKO-19 duniani ulisababisha kufungwa kwa safari za ndege na kusababisha kupungua kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini, kupunguza mikusanyo na kuathiri moja kwa moja pato la taifa.

"Hali hii pia ilichangia ukosefu wa fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya na kusababisha kuhaulisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya kutatua changamoto za afya na kupelekwa katika kukabiliana na UVIKO-19 na kuacha mahitaji mengine ambayo yalikuwa ni muhimu na yanaisaidia jamii moja kwa moja," alisema.

Alisema bajeti ya wizara yake imeathiriwa na uwapo wa janga la UVIKO-19 na kuwataka wajumbe wa Baraza hilo kuelewa upimaji wa virusi hivyo, Serikali ya Zanzibar haina uwezo wa kugharamia kwa wasafiri.

Naibu waziri huyo alisema wizara yake itaendelea na utaratibu wa sasa kufanya vipimo hivyo kwa malipo na unatumiwa na nchi zote duniani.




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa (kulia), akizungumza na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jenerali Mabeyo amuaga rasmi Mwinyi Ikulu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amempongeza Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Venance Mabeyo kwa kutekeleza vyema majukumu yake katika kipindi chake chote cha utumishi ndani ya jeshi hilo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati alipofanya mazungumzo na Mkuu huyo wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kumuaga kufuatia kumaliza muda wa utumishi wake ndani ya jeshi hilo mwishoni mwa mwezi huu.

Katika maelezo yake Rais Dk. Mwinyi alimwelezea Jenerali Mabeyo kuwa ni kiongozi aliyefanya kazi zake vyema katika jeshi hilo na kumpa ushirikiano mkubwa yeye na viongozi wenzake wakati akiwa Waziri wa Ulinzi hatua ambayo ilimwezesha kutekeleza mambo mengi ndani ya jeshi hilo.

Alisema ushirikiano alioupata kutoka kwa Jenerali Mabeyo wakati akiwa Waziri wa Ulinzi na hata akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anauthamini na ataendelea kuukumbuka.

Rais Mwinyi alimtakia kila la kheri Jenerali Mabeyo katika maisha yake ya kustaafu hasa ikikumbukwa kwamba amelitumikia kwa muda mrefu jeshi hilo na kufanya mambo mengi yatakayoacha alama.

Pia, alimpongeza kwa ushirikiano alioutoa katika kuhakikisha changamoto mbalimbali zinapatiwa ufumbuzi wakati wa uongozi wake ndani ya Jeshi hilo.

Alisifu hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zote mbili kwa ushirikiano wa Jeshi la Ulinzi Tanzania katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa changamoto za ardhi katika maeneo ya jeshi.

Alitoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya fidia hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa ufumbuzi wa kudumu katika changamoto hiyo.

Naye Mkuu wa Majeshi Mabeyo alitoa pongezi na shukrani kwa Rais Dk. Mwinyi kwa kutekeleza vyema uongozi wake uliotukuka tokea akiwa Waziri wa Ulinzi hadi hivi sasa akiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Jenerali Mabeyo alisema haja ya kumuaga pamoja na kutoa shukurani kwa Rais Dk. Mwinyi na kueleza kuwa ni kiongozi ambaye amefanya kazi naye kwa muda mrefu na kumsaidia katika kutekeleza vyema majukumu yake ndani ya jeshi hilo.

"Nakutakia afya njema na maisha marefu Mheshimiwa Rais pamoja na familia yako... nathamini sana ushirikiano ulionipa katika kipindi chako cha uongozi tokea ukiwa Waziri wa Ulinzi hadi leo hii, asante sana," alisema Jenerali Mabeyo.

Alisema kuwa Jeshi la Ulinzi Tanzania litaendelea kumkumbuka Rais Dk. Mwinyi kwa busara na hekima zake katika kuzishughulikia changamoto mbalimbali ndani ya Jeshi hilo ambalo hatimaye limepata mafanikio makubwa.

Kadhalika katika uongozi wake Rais Dk. Mwinyi akiwa Waziri wa Ulinzi alitatua changamoto kadhaa na kulifanyia mambo mengi jeshi hilo hatua ambayo imewafanya viongozi waendelee kufuata nyayo zake.

Alipongeza hatua zinazoendelea kuchukuliwa katika kutatua changamoto za ardhi na kueleza matarajio yake ya mafanikio yatakayopatikana katika kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hiyo.

Pia busara na hekima kubwa anayoendelea kutumia katika kuitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto hiyo ya ardhi hasa kwa kutambua kwamba jeshi ni sehemu ya wananchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUBADILISHA JINA



**KUANZIA TARAHE 26/5/2022 SITATUMIA TENA JINA LA ZAMANI LA FATUMA ABDALLAH THABITH BADALA YAKE NITATUMIA JINA LA SASA FATUMA ELIASA THABITH LINALOONEKANE KATIKA VYETI VYANGU VINGINE.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAGRETH MENKIRA MWENDE**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo cha certificate in accounting and finance kilichotolewa na Moshi Co- Operative University mwaka 2018. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa polisi: **KIL/MOS/RB/538984/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MATHIAS GERVASE RUTAGUZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya WANHOO yenye namba za usajili **MC 104 CUX.** Chassis No. **LWBHDNZ46LW045567.** Engine No. **WH170MMB201156854.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/190166/2022.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**ILIYOPO SHINYANGA**
**RUFAA YA JINAI NO.79 YA 2020**
**(ASILIA SHAURI LA JINAI NA.186 YA 2015 KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA BARIADI)**
**THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION**
**DHIDI YA NEEMA SAMSON**
**KWA; NEEMA SAMSON**

### POPOTE ULIPO

Unajulishwa kwamba mnamo tarehe 13/06/2022 saa 3;00 asubuhi imepangwa kusikilizwa kwa rufaa dhidi yako.

Hivyo unaamriwa kuhudhuria siku hiyo bila kukosa na kama hutahudhuria rufaa hiyo itasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama tarehe 06/06/2022

**M.P MRIO**
**HAKIMU MKAZI KUU**
**SHINYANGA**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 56/2022**
**In the matter of the Estate of the late AMANI YOHANA MFUNGWA of Ntyuka, within Dodoma Municipality.**
**AND**
**In the matter of the application for letters of administration by JONATHAN MFUGWA AND PENDO S. LYATI**

### GENERAL CITATION
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 08th Day of July, 2022

**Dated at Dodoma this 30TH day of March, 2022.**

............

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA.**

**MAOMBI NAMBA: 3/2022.**
**MATHEO AUGUSTINO KOMBA –MLETA MAOMBI.**

**DHIDI YA.**
**KASSIAN MAPUNDA –- MJIBU MAOMBI.**

### WITO/KUITWA SHAURINI.

Mjibu maombi uliotajwa hapo juu unaarifiwa kuwa shauri husika hapo juu,litatajwa katika Baraza hili hapo tarehe 4/7/2022 saa 2:30 asubuhi .Hivyo unatakiwa kuhudhuria bila kukosa ,binafsi au wakili wako au wote ,pamoja na ushahidi au utetezi unaotegemea shauri hili.

Kumbuka kwamba usipohudhuria shauri hilo litasikilizwa na kutolewa hukumu bila ya wewe kuwepo.

**Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27/05/2022.**

**MWENYEKITI.**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (WILAYA).**
**RUVUMA.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Usimamizi wa mirathi Na. 34/2022**
**MKOA DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TATU MOHAMED JUMA WA CHAMWINO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWAJUMA SALUM OMARY**

### TANGAZO
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 03 mwezi 06 mwaka 2022.**

---

**1FORM 58**

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.412 OF 2022**
**In The Matter Of the Estate of the Late...................BEATRICE JOHN SIJAONA**
**And**
**In The Matter Of Application for Letters Of Administration by**
**PATRICK JOHN SIJAONA**

### GENERAL CITATION
**(RULE 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 28th day **JUNE 2022**

**Dated at DAR ES SALAAM this 24th day of MAY 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Mnada utaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdhamini / Mdaiwa | Dhamana / Mahali ilipo | Tarehe ya mnada / Dalali |
|---|---|---|
| Matiku Mgaya Masabi / Miriam John Mallya | Nyumba - Kigilagila -Dsm | 28.06.2022 ( Tausi A/Mart ) |
| Abdalall Husein Waziri/Khadija Husein .Jafarah | Nyumba – Mtaa wa Kombo Vingunguti Dsm | 23.06.2022 - Champion A/Mart |
| Delly Juma Waziri/ Aloyce John Mnyari | Nyumba – Msimbazi Magharibi - Dsm | 24.06.2022 - Champion A/Mart |

**Masharti:**

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**TAUSI Auction Mart: 0719351040/0692926969**
**CHAMPION A/Mart :0652666279/0718756119**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Korea Kusini, Marekani zarusha makombora kutoa onyo K. Kaskazini

**SEOUL,** Korea Kusini

RAIS wa Korea Kusini Yoon Suk-yeol, amesema nchi yake itajibu kwa ukali uchokozi wowote kutoka Kaskazini.

Baada ya kauli hiyo, nchi hiyo ikishirikiana na Marekani zilirusha makombora manane jana, kujibu msururu wa makombora ya balistiki yaliyorushwa na Korea Kaskazini hivi karibuni.

Rais Suk-yeol alisema serikali yake itajibu vikali chokochoko zozote kutoka kwa jirani yake wa kaskazini.

"Tutahakikisha hakuna ufa hata mmoja katika kulinda maisha na mali ya watu wetu," alisema.

Akizungumza katika hafla ya kumbukumbu ya vita huko Seoul, aliongeza kuwa mipango ya nyuklia na makombora ya Korea Kaskazini inafikia kiwango cha kutishia sio tu amani kwenye Rasi ya Korea, lakini pia Kaskazini Mashariki mwa Asia na ulimwengu.

Marekani na Korea Kusini mara kwa mara hufanya mazoezi ya pamoja ya kijeshi, ambayo mara nyingi huikasirisha Korea Kaskazini.

Mapema Jumatatu, saa chache baada ya Korea Kaskazini kurusha makombora kadhaa kwenye pwani yake ya mashariki, washirika hao wawili walirusha kujibu mashambulizi.

Wachambuzi wanasema hatua hiyo ni ya Korea Kusini kuonyesha uwezo wake, kwa usaidizi wa silaha za Marekani.

Hili ni tukio la pili la kulipiza kisasi kutoka kwa Marekani na Korea Kusini ndani ya wiki kadhaa, huku hatua sawa na hiyo ikifanywa wiki iliyopita baada ya Korea Kaskazini kurusha makombora mara Rais wa Marekani Joe Biden, kumaliza ziara yake nchini humo. **BBC**



# Uingereza kutuma makombora masafa marefu kuilinda Ukraine

**LONDON,** Uingereza

WAKATI Uingereza inatuma makombora yake ya kwanza ya masafa marefu nchini Ukraine, Russia imesafirisha vifaa vyake vya ulinzi katika kisiwa kimoja kwa ajili ya kujilinda.

Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo, Ben Wallace, alisema mfumo wa roketi wa M270 utasaidia Ukraine kujilinda dhidi ya Russia.

Serikali ya Uingereza haijathibitisha ni silaha ngapi zitapelekwa Ukraine kama msaada, lakini BBC inafahamu kuwa mwanzoni zitakuwa tatu.

Uamuzi huo uliratibiwa na Marekani, ambayo ilitangaza wiki iliyopita pia kuwa inasambaza mfumo wa makombora. Hatua hiyo ya Marekani tayari imeikasirisha Russia na kumfanya Rais Vladimir Putin kutishia kuongeza orodha ya maeneo ambayo itashambulia nchini Ukraine ikiwa nchi za Magharibi zitapeleka silaha za masafa marefu Kyiv.

Serikali ya Uingereza ilisema kuwa wanajeshi wa Ukraine watapewa mafunzo ya jinsi ya kutumia virutubishi nchini Uingereza katika wiki zijazo.

Akitangaza hatua hiyo, Wallace alisema Uingereza ilikuwa ikichukua nafasi kubwa katika kuwapa wanajeshi wa Ukraine silaha muhimu wanazohitaji ili kulinda nchi yao dhidi ya uvamizi wa Russia.

"Kadiri mbinu za Russia zinavyobadilika, ni lazima uungwaji mkono wetu kwa Ukraine ufike mbali, mifumo hii yenye uwezo mkubwa wa kurusha roketi itawawezesha marafiki zetu wa Ukraine kujilinda vyema dhidi ya matumizi ya kikatili ya mizinga ya masafa marefu, ambayo majeshi ya Putin yametumia kiholela kushambulia miji," alisema.

**Huenda, silaha hizi zimetengenezwa kwa ajili ya kutoa ulinzi wa mashambulio ya anga kwa meli za kivita za Russia karibu na kisiwa cha Zmeiny.**

Mfumo wa Uingereza wa kurusha roketi nyingi unaweza kurusha makombora 12 kutoka ardhini kwenda angani ndani ya dakika moja na unaweza kulenga shabaha ndani ya maili 50 sawa na km 80 kwa usahihi.'

Kifaa hicho ni sawa na mfumo ambao Marekani inatuma wa aina ya M142 High Mobility Artillery Rocket System (HIMARS).

Russia yahamishia mifumo ya ulinzi kisiwani.

Hata hivyo, kulingana na taarifa za ujasusi wa Uingereza, mifumo ya ulinzi ya Russia inapelekwa katika kisiwa cha Nyoka.

Ujumbe wa ujasusi wa kijeshi wa Uingereza unaoripoti kuhusu Ukraine, ulisema kuwa baada ya kupoteza meli ya Moskva, jeshi la Russia limehamisha mifumo yao ya ulinzi wa mashambulizi ya anga katika kisiwa hicho kilichoko katika Bahari nyeusi.

"Huenda, silaha hizi zimetengenezwa kwa ajili ya kutoa ulinzi wa mashambulio ya anga kwa meli za kivita za Russia karibu na kisiwa cha Zmeiny," ilisema taarifa hiyo.

Inaeleza kwamba hatua za jeshi la Russia karibu na Zmeinoye zilisaidia kufunga eneo la mwambao wa Ukraine na kuzuia kuanzishwa tena kwa biashara ya majini, ikiwamo kusafirisha nafaka nje ya Ukraine.

Ukraine na nchi za Magharibi wanaishutumu Russia kwa kuzuia mauzo ya nje ya chakula kutoka katika bandari za nchi hiyo.

Nchi nyingi duniani hutegemea nafaka kutoka Ukraine, ambapo ukosefu wake unatishia baa kubwa la njaa.

Taarifa ya mkuu wa ujasusi wa Uingereza pia ilisema kuwa Jumapili asubuhi Russia ilifanya shambulio la kombora kutoka majini la Kh-101 kwenye miundombinu ya reli mjini Kyiv.

Russia inadai kwamba shambulio la Jumapili katika mji wa Kyiv liliharibu vifaru vilivyotolewa na nchi za Magharibi kwa Ukraine. Lakini kulingana na serikali ya Ukraine, kiwanda cha ukarabati wa magari ndio kilichoharibiwa kidogo, na kwamba hapakuwa na zana za kijeshi.

Maofisa wa Ukraine waliwaalika waandishi wa habari kwenye kiwanda hicho na kuwaonyesha kiwango cha uharibifu uliofanyika.

Kuhusu hali katika jimbo la Donbass, Uingereza iliandika kuwa mapigano makali yanaendelea katika mji wa Severodonetsk.

Vikosi vya Russia vimeendelea na mashambulizi vikisonga mbele kuelekea Sloviansk, vikijaribu kuzingira vikosi vya Ukraine. **BBC**



Waokoaji wakijaribu kuendelea na shughuli ya uokozi usiku, wakati mkasa wa kukwama kwa wachimba migodi ulipotokea Mei nchini Burkina Fasso. **PICHA: BBC**

# Nigeria yaharibu pikipiki 2,000 za usafiri

**Lagos,** NIGERIA

ZAIDI ya pikipiki 2,000 zilizokamatwa na polisi zimeharibiwa nchini Nigeria baada ya serikali kupiga marufuku usafiri wa vyombo hivyo maarufu kama okada.

Hatua hiyo imetokana na tukio la kushambuliwa kwa mwanamume mmoja na watu wanaoshukiwa kuwa waendeshaji pikipiki mwezi uliopita.

Katika tukio hilo, Sunday David, ambaye ni mhandisi wa sauti mwenye umri wa miaka 38, aliuawa katika mtaa wa soko la Lekki baada ya kutofautiana kuhusu nauli.

Kifo chake kilizua hasira na kuwalazimu mamlaka ya jiji la Lagos, kuchukua hatua ya kupiga marufuku uchukuzi huo.

Marufuku hiyo ilizua maoni tofauti kutoka kwa wakazi wa eneo hilo huku wengine wakisema wahudumu wa pikipiki hizo huziendesha kwa njia hatari, huku wengine wakisema kuendesha okada kunatoa ajira muhimu kwa vijana.

Fundi anayeishi Ikeja, Wasiu Adekoya, alisikitishwa na unyonge wa waendeshaji okada.

"Wao wanateka nyara watu. Kile ambacho serikali ilifanya ni sawa. Hatutaki matatizo katika jimbo la Lagos," alisema. **DW**

## HABARI MICHEZO

# CRDB BANK MARATHON 2022 KUTIMUA VUMBI AGOSTI DAR

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya riadha ya Benki ya CRDB maarufu kwa jina la CRDB Bank Marathon ya msimu wa tatu yamepangwa kufanyika Agosti 14, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

**Mbio hizo zinatarajiwa kushirikisha washiriki zaidi ya 6,000, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Ester Mwambapa.**

Mwambapa aliliambia Nipashe juzi kuwa mashindano hayo yatashirikisha wanariadha wa ndani na nje ya nchi wanawake na wanaume na pia kutakuwa na mbio za baiskeli za kilometa 65 ambazo zitashirikisha jinsia zote.

Alizitaja mbio hizo kuwa ni marathon, nusu marathon, kilometa 10 na kilometa tano, ambapo wakimbiaji watapita mbele ya makao makuu mapya ya CRDB Bank "The Iconic Building" na katika daraja la fahari ya Jiji la Dar es Salaam na Tanzania, Tanzanite.

Alifafanua kuwa mbizo hizo zinatambulika kimataifa kupitia Chama cha Kimataifa cha Mbio Ndefu na Fupi za Marathon (AIMS) na Shirikisho la Mchezo huo duniani (WA).

"Maandalizi yameanza kwa washiriki kujisajili na fedha zote zitakazokusanywa zitatumika kusaidia matibabu ya watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na matibabu ya watoto na kinamama katika Hospitali ya CCBRT," alisema Mwambapa.

Alisema kuwa kaulimbiu ya mbio za mwaka huu ni "Hii ni Kubwa Kuliko" katika mbio hizo ambazo zitaanzia na kumalizikia katika viwanja vya Farasi, Oysterbay maarufu kwa jina la The Greens.

Kwa upande wa Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mohamed Mchengerwa, akizungumza wakati wa uzinduzi rasmi wa mbio hizo za mwaka huu, mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuendeleza mbio hizo na kuleta msisimko katika maendeleo ya michezo hapa nchini mbali ya kujenga afya na kusaidia jamii.

Mchengerwa alisema kuwa serikali imefarijika kuona kuwa mbio hizo zinazidi kukua na kuleta tija kwa jamii na kuwaomba washiriki kujisajili ili kufanikisha mbio hizo.

"Nichukue fursa hii kuipongeza Benki ya CRDB kwa kuhamasisha maendeleo ya michezo, afya na kusaidia jamii kupitia michezo. Naamini washiriki watakuwa wengi zaidi katika mbizo hizi," alisema Mchengerwa.

Uzinduzi wa mbio hizo pia ulipambwa na wakimbiaji watatu waliokimbia kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma kwa siku tatu kama sehemu ya kuhamasisha mbio hizo. Wakimbiaji hao ni Joseph Katembo, Edson Mwakalukwa, na Patrick Katemba.




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (wa tatu kushoto), akipokea bendera ya CRDB Bank Marathon kutoka kwa mashujaa watatu waliokimbia kutoka jijini Dar es Salaam makao makuu ya Benki ya CRDB hadi jijini Dodoma kwa siku tatu ikiwa ni adhimisho la ufunguzi rasmi wa msimu wa tatu tangu kuanzishwa kwa mbio hizo. Wengine Pichani ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB shujaa wa uanzishwaji wa mbio hizo, Tully Esther Mwambapa (kushoto), Patrick Katemba, Edson Mwakalukwa, Joseph Katembo na Kaimu Meneja wa Kanda ya Kati wa Benki ya CRDB, Jane Maganga (kulia). Uzinduzi wa usajili huo ulifanyika jijini Dodoma Jumamosi iliyopita, ambapo mbio hizo zinatarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam Agosti 14, mwaka huu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mafunzo, Kipanga kuumana FA leo*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NUSU fainali ya pili ya Kombe la FA inatarajia kupigwa leo katika Uwanja wa Amaan ikiwakutanisha Maafande wa Mafunzo dhidi ya Maafande wa Kipanga kwa upande wa Kanda ya Unguja.

Katika nusu fainali ya kwanza Kanda ya Pemba iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Gombani, Chipukizi ilifanikiwa kutangulia fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi Tekeleza FC, hivyo sasa inasubiri mshindi wa leo kukutana fainali na bingwa wa ataiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa timu ya Kipanga, Khamis Hassan, alisema wamejiandaa kushinda na kutinga fainali ya michuano hiyo baada ya muda mrefu kutoshiriki michuano ya kimataifa.

Alisema kutokana na kufikia hatua hiyo, watahakikisha wanatimiza lengo lao la kuwa wawakilishi wa Zanzibar katika michuano ya kimataifa.

Hassan alisema wachezaji wake wote wanaendelea vizuri na nyota wake wote wa kikosi cha kwanza wapo tayari kwa mechi hiyo.

Alisema matarajio yao makubwa ni kuona wanashinda na kuwa wawakilishi wa nchi katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Kwa upande wa Kocha wa Timu ya Mafunzo, Mohamed Abdallah, ambaye ndio mabingwa watetezi wa kombe hilo, alisema wanashuka dimbani leo wakiwa na lengo moja tu la kuutetea ubingwa wao.

Kocha huyo alisema wamejiandaa kushinda na kuwa wawakilishi wa Zanzibar katika michuano Kombe la Shirikisho Afrika kwa mara ya pili mfulululizo.

Alisema anatumai mashabiki wengi watahudhuria mechi hiyo na kuongeza hamasa ya ushindi kwa kikosi chake.

# TPLB yafafanua majina CAF Juni 30

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Tanzania (TPLB), imewatoa hofu mashabiki wa soka nchini kuwa itatuma majina ya wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano inayoendeshwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ndani ya muda, huku ikifafanua kuwa yanayotakiwa kutumwa mwishoni mwa Juni 30 ni ya timu na wala si wachezaji.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo amesema hayo kufuatia hofu iliyowashika mashabiki wengi wa soka nchini baada ya CAF kutangaza kuwa Juni 30 ndiyo mwisho wa kutuma majina kwa timu zote zitakazoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Wengi walidhani kuwa ni majina ya wachezaji, lakini Bodi ya Ligi imesema kinachotakiwa kutumwa ni majina ya timu zinazotakiwa kushiriki michuano hiyo na wao watatekeleza hilo ndani ya muda, licha ya kwamba mechi ya fainali ya Kombe la FA itachezwa Julai 2, mwaka huu, ambayo ni nje ya muda uliowekwa na shirikisho hilo.

"Hili siyo tatizo na bahati nzuri tumewasiliana nao, tupo ndani ya utaratibu kwa mawasiliano tuliyoyafanya na wenzetu. Hii si mara ya kwanza kutokea duniani, kwa bahati ni kwamba Ligi Kuu itakwisha siku moja kabla ya siku ya kutuma majina, huku kwenye Kombe la FA sisi tutapeleka jina la Yanga pamoja na Coastal Union kuna mmoja wapo atakuwa mwakilishi kwenye michuano ya Kombe la FA, lakini itategemea na matokeo ya fainali, kama nilivyosema hili hufanyika kote duniani, mfano mshindi wa A vs B, ndiyo atakuwa mwakilishi," alisema.

Kasongo alisema kwenye kanuni ya msimu huu, ni kwamba bingwa wa Kombe la FA, kama atakuwa ni bingwa wa Ligi Kuu ambao ni Yanga, basi Coastal Union watakosa nafasi, na badala yake washindi wanne wa juu wa Ligi Kuu Tanzania Bara wataiwakilisha nchi, wa kwanza na wa pili Ligi ya Mabingwa na wa tatu na nne watacheza Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kama Coastal atashinda, basi atacheza CAF na kwenye Ligi Kuu wawakilishi watakuwa watatu tu, hiyo yote tumezingatia ndiyo maana tutapeleka majina ya timu zote mbili, lakini tutaeleza haya ambayo yapo kwenye kanuni zetu," alisema Kasongo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### SALAH ATAKIWA BARCA

BARCELONA wamemwambia mshambuliaji wa Liverpool na timu ya taifa ya Misri, Mohamed Salah, 29, kwamba anaweza kujiunga nao kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake na wekundu hao utakapomalizika msimu ujao. ***(Mirror)***

#### SPENCE AWANIWA



KLABU ya Tottenham Hotspur wanajiandaa kuongeza juhudi za kumsaka beki wa Middlesbrough, Djed Spence, 21, ambaye alikuwa Nottingham Forest kwa mkopo wa msimu mzima. ***(Express)***

#### GAVI BASI TENA

LIVERPOOL wamesitisha mpango wao wa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Barcelona mwenye umri wa miaka 17 raia wa Hispania, Gavi. ***(Sport)***

#### MATIC NA ROMA



KIUNGO wa kati wa Serbia, Nemanja Matic, 33 atajiunga na AS Roma kwa uhamisho huru mara mkataba wake utakapomalizika kule Manchester United mwisho wa mwezi huu wa Juni. ***(Sky Sports)***

#### NEMANJA KUTOSWA

AS Roma inaweza kusitisha juhudi za kumsaka Nemanja Matic ikiwa itafanikiwa kumnunua kiungo wa kati wa Aston Villa na Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24. ***(Mail)***

#### GOTZE HUYO BENFICA



KLABU ya Benfica ina matumaini ya kufikia makubaliano na mchezaji wa kimataifa wa zamani wa Ujerumani, Mario Gotze mwenye umri wa miaka 30, kuhusu uhamisho kutoka PSV. ***(Fabrizio Romano)***

#### RICE KUREJEA

CHELSEA huenda ikasaidia kumshawishi mchezaji wao Declan Rice mwenye umri wa miaka 23, kurejea nyumbani kutoka klabu ya West Ham kwa kumpatia kiungo huyo wa kati wa England. ***(Express)***

#### RAPHINHA NA BARCA



MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Mateu Alemany anatarajia kwenda England kuanza mazungumzo na Leeds United kuhusu mpango wa kumsajili fowadi wa Brazil, Raphinha, 25. ***(Sport, via Mail)***.

#### DE LIGT NA JUVE

MLINZI wa Uholanzi, Matthijs de Ligt, 22, amethibitisha kuwa yuko kwenye mazungumzo na Juventus kuhusu mkataba mpya. ***(90min)***

#### LODI AWANIWA



KLABU ya Newcastle wamemfanya mlinzi wa Atletico Madrid raia wa Brazil, Renan Lodi, 24, kuwa chaguo lao la kwanza kuziba pengo la beki wa kushoto. (Jacque Talbot, ***Give Me Sport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI ATUPIA 5 ARGENTINA 'IKIUA', SCALONI APAGAWA

**Yeye ni urithi wa dunia, wa soka la dunia, siku ambayo hatacheza tena, tutammisi sana...**

**POMPLONA,** Hispania

LIONEL Messi alifananishwa na Rafael Nadal na kocha wake Lionel Scaloni baada ya kufunga mabao yote matano ya Argentina katika mechi ya kirafiki ya ushindi wa 5-0 dhidi ya Estonia, Jumapili.

**Gwiji huyo wa zamani wa Barcelona, Messi alifikisha mabao 86 ya kimataifa, mawili zaidi ya gwiji wa Hungary, Ferenc Puskas, na hivyo kumweka nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji wa muda wote wa timu ya taifa.**

Ushujaa wa Messi ulifanyika siku moja wakati nguli wa tenis, Nadal alipomshinda Casper Ruud kwa seti mfululizo na kushinda taji la 14 la French Open na kuendeleza rekodi yake ya kufikisha mataji makubwa 22.

Kwa bosi wa Argentina, Scaloni, hakuna sifa bora zaidi zilizobaki kwake kuelezea mchango wa Messi katika ulimwengu wa soka.

"Sijui niseme nini tena. Ni ngumu sana; ni kama Rafa Nadal, utasema nini?" Alisema Scaloni akiiambia TVP.

"Inapendeza zaidi kwamba waandishi wa habari waseme, wazungumze. Huna maneno ya kutosha zaidi kuelezea hali hii."

Matokeo hayo yaliifanya Argentina kuendeleza mbio zao za kutopoteza michezo hadi 33, ikiwa ni kiwango kizuri zaidi miezi mitano tu kabla ya kuanza kwa Kombe la Dunia nchini Qatar.

Messi alikuwa amekamilisha hat-trick yake mapema katika kipindi cha pili kabla ya kufunga mabao mawili zaidi katika dakika 20 za mwisho.

Scaloni aliongeza: "Yeye ni kitu cha kipekee, na ni furaha kuwa naye katika kundi hili. Ni furaha kumfundisha na hata makocha wengi wanapenda kuwa naye.

"Tuna maneno tu ya shukrani. Sidhani kama yeye ni urithi wa Argentina; yeye ni urithi wa dunia, wa soka la dunia. Siku ambayo hatacheza tena, tutammisi sana."

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,004,0

JACKPOT

MECHI WIKI HII

TAREHE: 7-9 JUNI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.07/06/22 | 21:45 | Germany vs England | 2.37 | 3.19 | 2.99 |
| 02.07/06/22 | 21:45 | Faroe Islands vs Luxembourg | 3.58 | 3.12 | 2.13 |
| 03.07/06/22 | 21:45 | Bosnia and Herzegovina vs Romania | 2.19 | 3.28 | 3.23 |
| 04.08/06/22 | 01:00 | Vila Nova GO vs Brusque SC | 2.15 | 2.99 | 3.33 |
| 05.08/06/22 | 01:00 | Nautico PE vs Vasco da Gama | 2.60 | 2.85 | 2.75 |
| 06.08/06/22 | 03:30 | Cuiaba MT vs Corinthians | 3.04 | 2.89 | 2.35 |
| 07.08/06/22 | 21:45 | Ireland vs Ukraine | 2.30 | 3.17 | 3.12 |
| 08.09/06/22 | 01:00 | America Mineiro MG vs Ceara CE | 2.38 | 2.95 | 2.95 |
| 09.09/06/22 | 01:00 | Juventude RS vs Atletico Pr | 2.55 | 2.90 | 2.75 |
| 10.09/06/22 | 03:30 | Santos vs Internacional | 2.34 | 3.00 | 2.95 |
| 11.09/06/22 | 21:45 | North Macedonia vs Georgia | 2.19 | 3.09 | 3.45 |
| 12.09/06/22 | 21:45 | Malta vs Estonia | 2.29 | 3.03 | 3.29 |
| 13.09/06/22 | 22:15 | UMF Grindavik vs Fjolnir | 2.60 | 3.63 | 2.28 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa





# MANE NJIA PANDA LIVERPOOL

**DAKAR,** Senegal

SADIO Mane amesisitiza kuwa anaiheshimu Liverpool, lakini hawezi kuthibitisha kwamba atabakia hapo huku akihusishwa na Bayern Munich.

Mshambuliaji huyo wa Liverpool amekuwa akihusishwa sana na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na alisema angeweka wazi kuhusu mustakabali wake baada ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid wiki iliyopita.

Mane hakutoa ufafanuzi juu ya mustakabali wake baada ya kufungwa na Madrid, lakini akasema mpango wake ni kuondoka kwenye Ligi Kuu England na atawaruhusu watu wa Senegal kuamua hatima yake.


"Ni kati ya asilimia 60 hadi 70 ya Wasenegal wanataka niondoke Liverpool? Nitafanya wanavyotaka. Tutaona hivi karibuni," alisema akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa, Ijumaa.

Lakini baada ya kuwa mfungaji bora wa Senegal kwa kufunga hat-trick dhidi ya Benin Jumamosi, Mane alirudia maoni yake huku akieleza jinsi anavyoifurahia Liverpool.

"Nilizungumza huku nikitania kwa ucheshi kidogo. Nadhani tutaishia hapo," aliiambia Canal Plus.

"Liverpool ni klabu ninayoiheshimu sana. Mashabiki walinikubali tangu siku ya kwanza. Kuhusu siku zijazo, tutaona."

Mane aliichezea Liverpool mechi 51 katika msimu wa 2021-22 na kufunga mabao 23 na kusaidia mengine mawili kwenye mashindano yote.




## Rais Bayern anaamini Lewandowski atabaki

**MUNICH,** Ujerumani

RAIS wa Bayern Munich, Herbert Hainer ametangaza kuwa "anajiamini" Robert Lewandowski atabakia msimu ujao, licha ya kuhusishwa na Barcelona.

Lewandowski na mabingwa hao wa Bundesliga wameingia kwenye mzozo kuhusu mkataba mpya, huku nyota huyo wa Bayern akidai hakuna ofa mpya ambayo imewekwa ili kuongeza muda wake wa kukaa hadi mwisho wa mkataba wake wa sasa, ambao unamalizika Juni 2023.

Hata hivyo, Bayern wamebainisha kuwa "ofa halisi" iko mezani huku Barcelona wakiwa kwenye mbio za kuinasa saini ya Lewandowski, ambaye ameweka wazi upendeleo wake wa kujiunga na miamba hao wa LaLiga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland alitangaza kwamba, historia yake na kikosi hicho cha kocha Julian Nagelsmann ilikuwa imekamilika mwishoni mwa Mei, lakini Rais Hainer bado ana matumaini kwamba Bayern itambakisha mshambuliaji huyo.

Hainer aliliambia BILD: "Mkataba ni mkataba! Tunaenda wapi ikiwa mchezaji anaweza kumaliza mkataba kabla ya wakati wake wakati sisi kama klabu tutamlipa hadi siku ya mwisho ya muda wake?



055,092/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.11/06/22 | 19:00 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.31 | 2.90 | 3.30 |
| 02.11/06/22 | 19:00 | Ireland vs Scotland | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 03.11/06/22 | 21:30 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 04.11/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 05.11/06/22 | 22:00 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 06.11/06/22 | 22:00 | Girona vs Tenerife | 2.32 | 3.10 | 3.05 |
| 07.12/06/22 | 00:00 | Sarmiento vs Argentinos Juniors | 3.05 | 3.15 | 2.28 |
| 08.12/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Bragantino SP | 2.80 | 3.05 | 2.55 |
| 09.12/06/22 | 02:30 | Tombense MG vs CSA AL | 2.70 | 2.75 | 2.90 |
| 10.12/06/22 | 03:00 | Internacional vs Flamengo | 2.80 | 3.30 | 2.37 |
| 11.12/06/22 | 07:00 | Renofa Yamaguchi vs Fagiano Okayama | 3.05 | 2.95 | 2.44 |
| 12.12/06/22 | 08:00 | Mito Hollyhock vs Montedio Yamagata | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 13.12/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Omiya Ardija | 2.41 | 3.00 | 3.05 |
| 14.12/06/22 | 19:00 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.43 | 2.95 | 3.05 |
| 15.12/06/22 | 21:30 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.47 | 3.25 | 2.75 |
| 16.12/06/22 | 22:00 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 17.12/06/22 | 22:00 | Sporting Kansas City vs New England Revolution | 2.85 | 3.40 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 07/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4273 | Egersund IK vs Notodden | 1.30 | 5.49 | 6.66 |
| 15:00 | 4428 | Odder Igf vs Ringkobing IF | 2.01 | 3.70 | 3.01 |
| 15:00 | 5467 | Volda vs Lillehammer FK | 1.84 | 3.83 | 3.39 |
| 15:00 | 5980 | FC Einheit Wernigerode vs Einheit Rudolstadt | 2.09 | 3.42 | 3.03 |
| 16:00 | 1380 | SV 1914 Eilendorf vs SV Deutz 05 | 1.29 | 5.32 | 7.29 |
| 16:00 | 1584 | Kvik Halden vs Sotra | 1.60 | 4.10 | 4.30 |
| 16:00 | 2326 | Honefoss vs Forde | 1.99 | 3.87 | 2.94 |
| 16:00 | 2561 | Viktoria Arnoldsweiler vs VfL Alfter | 2.51 | 4.03 | 2.20 |
| 16:00 | 3436 | Vindbjart vs Sarpsborg Sparta 2 | 1.86 | 4.03 | 3.19 |
| 16:00 | 3850 | SV 1910 Breinig vs VfL Vichttal | 8.04 | 6.27 | 1.23 |
| 16:00 | 4147 | Bor. Freialdenhoven vs Hennef 05 | 3.88 | 4.61 | 1.60 |
| 16:00 | 4723 | Japan U23 vs Saudi Arabia U23 | 2.45 | 2.99 | 2.79 |
| 16:00 | 4726 | Bergisch Gladbach vs 1. FC Duren | 2.80 | 3.49 | 2.19 |
| 16:00 | 4883 | Eidsvold Turn vs Asker | 2.07 | 3.54 | 3.00 |
| 16:00 | 5882 | Eik-Tonsberg vs Halsen IF | 1.45 | 4.93 | 4.83 |
| 16:30 | 1370 | Spvg Frechen 20 vs FC Hurth | 1.58 | 4.23 | 4.32 |
| 16:30 | 5362 | Siegburger SV 04 vs FC Pesch | 1.99 | 3.63 | 3.09 |
| 17:00 | 1350 | Strindheim IL vs Trygg/Lade | 1.22 | 6.50 | 7.88 |
| 17:00 | 1683 | Gjellerasen vs Floya | 1.37 | 5.10 | 5.69 |
| 17:00 | 3624 | Baerum vs Kjelsaas | 2.88 | 3.47 | 2.15 |
| 17:00 | 4117 | Odds BK 2 vs Moss | 3.93 | 3.93 | 1.69 |
| 17:00 | 4464 | Harstad vs Mjondalen 2 | 2.89 | 4.40 | 1.90 |
| 17:00 | 4621 | Start 2 vs Mandalskameratene | 4.12 | 4.81 | 1.54 |
| 17:00 | 4869 | Orn-Horten vs Strommen | 2.74 | 3.38 | 2.27 |
| 18:30 | 2522 | TPS Turku vs PK-35 | 1.48 | 3.94 | 5.91 |
| 20:00 | 1552 | Mbour Petite Cote vs ASC Jaraaf | 5.31 | 3.00 | 1.73 |
| 20:00 | 1921 | US Goree vs AS Douanes | 1.86 | 2.90 | 4.62 |
| 20:00 | 2100 | AS Dakar Sacre Coeur vs Generation Foot | 3.53 | 2.64 | 2.28 |
| 20:00 | 3105 | Teungueth vs Casa Sport | 2.81 | 2.46 | 2.96 |
| 20:00 | 5143 | Cneps vs ASC Diambars | 1.73 | 3.34 | 4.52 |
| 20:00 | 5536 | Asec Ndiambour vs AS Pikine | 2.00 | 2.80 | 4.12 |
| 21:30 | 2076 | Justo Jose De Urquiza vs Villa San Carlos | 2.75 | 2.79 | 2.65 |
| 21:30 | 4138 | Deportivo Riestra vs Deportivo Madryn | 2.45 | 2.75 | 3.04 |
| 21:30 | 5408 | Deportivo Muniz vs Argentino Rosario | 2.90 | 2.60 | 2.70 |
| 21:30 | 5623 | Deportivo Paraguayo vs Central Ballester | 3.33 | 2.75 | 2.29 |
| 21:45 | 1618 | Slovakia vs Kazakhstan | 1.26 | 5.23 | 12.06 |
| 21:45 | 3619 | Andorra vs Moldova | 3.93 | 2.97 | 2.09 |
| 21:45 | 4019 | Austria vs Denmark | 2.58 | 3.24 | 2.68 |
| 21:45 | 4256 | Belarus vs Azerbaijan | 2.97 | 2.92 | 2.56 |
| 21:45 | 4607 | Iceland vs Albania | 2.88 | 2.98 | 2.58 |
| 21:45 | 4805 | Croatia vs France | 3.38 | 3.43 | 2.07 |
| 22:00 | 2935 | Equatorial Guinea vs Libya | 2.13 | 2.98 | 3.78 |
| 23:00 | 1646 | Bonaire vs Sint Maarten | 1.22 | 5.88 | 8.82 |
| 14:30 | 3854 | Hangzhou NG vs Changchun Yatai | 4.42 | 3.64 | 1.67 |
| 15:00 | 2296 | Molde FK 2 vs Kongsvinger 2 | 1.33 | 5.50 | 6.09 |
| 16:00 | 3481 | Australia U23 vs Jordan U23 | 1.96 | 3.08 | 3.77 |
| 16:00 | 4432 | Iraq U23 vs Kuwait U23 | 1.49 | 3.78 | 6.08 |
| 16:00 | 5583 | Finland U21 vs Azerbaijan U21 | 1.21 | 5.51 | 10.83 |
| 16:30 | 2632 | Machine Sazi Tabriz vs Shahin Bushehr | 2.39 | 2.75 | 3.35 |
| 17:30 | 3366 | Esteghlal Mollasani vs Arman Gohar Sirjan | 2.06 | 2.80 | 3.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MBUNGE ATAKA MSHAHARA WACHEZAJI UANZIE MILIONI 1

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MBUNGE wa Jimbo la Makete, Festo Sanga (pichani), amesema mpira wa Tanzania una safari ndefu kutokana na uwekezaji hafifu na malipo duni kwa wachezaji.

**Aidha, alitaka uwapo utaratibu wa kuwalipa wachezaji mishahara mizuri kwa kuwa wengi wanamalipo dunia kiasi cha kuonyesha kuwa vipaji vyao havithaminiwi.**

Akichangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema bila kuchukua hatua madhubuti nchi itashindwa kujitambulisha vema duniani.

"Lazima kuweka viwango vya mishahara kwa wachezaji wa Ligi Kuu, Daraja la Kwanza na Timu za Taifa. Vijana wetu wanacheza wanalipwa 200,000 au 300,000," alisema na kuongeza:

"Vijana wetu wanacheza kwa jasho sana wakipata magonjwa tunaishia kuwachangia, lazima tuweke kiwango cha mishahara mchezaji wa Ligi Kuu kima cha chini kiwe Sh. milioni moja kwenda juu, tuna fedha nyingi kwenye mpira zinapotea. Leo tunawapigia makofi Serengeti Girls, lakini hawana hata 200,000 mfukoni.

"Mpira wetu una safari ndefu, mfumo tunaoenda nao ni wa zimamoto, tunatamani kuwa na matokeo mazuri, lakini hatutajenga msingi ya kuzalisha wachezaji. Tunafurahia Serengeti Girls wanaenda kucheza Kombe la Dunia, lakini hatujui wamefikaje huko na hatujaanda wengine wa baadaye,"alisema.

Aidha, alisema Zanzibar ina 'module' (mpangilio) nzuri ya maendeleo ya mpira Afrika Mashariki Tanzania na Afrika, ambayo ilichukuliwa na kutumiwa na Cameroon na Ghana, ikaleta matokeo makubwa.

"Kwenye taifa lolote dunia lazima nchi ijipambanue nini inataka kwenda nacho leo nikitaja Marekani ni mpira wa kikapu, Brazili ni Samba Soka, Kenya ni riadha, Burundi ni makocha, makocha wa timu kuu wote ni Warundi, Rwanda ni basketball, sisi Tanzania tunajiangalia wapi,"alihoji.

Alisema sheria namba moja ya Shirikisho la Mpira duniani (FIFA) inataka tuwe na viwanja ndiyo mpira uchezeke, taifa letu viwanja vimekuwa changamoto kubwa, kwa kuwa vimegeuka vya shughuli nyingine na siyo mpira.

Alisema anajiuliza lengo la Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kujenga viwanja nchi nzima ilikuwa vigeuke kuwa magofu au mazizi ya ng'ombe, alijenga viwanja kwa ajili ya michezo, na kwamba utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan, itekelezwe kwa kuendeleza viwanja vya mpira kwa kuweka nyasi bandia na kuvifanya vitumike.

Alisema bajeti imetenga bilioni 10 kwa ajili ya ukarabati, na kwamba Ligi Kuu haihitaji ukarabati wa viwanja pekee, bali kuweka nyasi bandia, na kwamba Nyerere alijenga akiwa na Watanzania milioni 20 na sasa tuko milioni 60 tumeshindwa kuviendeleza.

Mbunge Sanga alisema mwaka 2027 Tanzania inataka kuwa mwenyeji wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), tutakuwa mwenyeji vipi kwa viwanja hivi.



# Biashara yatimua benchi la ufundi

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Timu ya Biashara United umewafuta kazi benchi lake la ufundi kuanzia Kocha Mkuu, Vivier Bahati kutokana na misuguano ya wenyewe kwa wenyewe na matokeo mabovu ya timu hiyo kwenye msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Biashara United inashika nafasi ya 15, ya pili kutoka mkiani katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Akizungumza na gazeti hili jana, Vivier Bahati alikiri kupewa barua ya kufutwa kazi pamoja na msaidizi wake pamoja na meneja wa timu hiyo baada ya viongozi hao kukutana na kuafikiana na uamuzi huo.

Alisema viongozi hao walikutana tangu Juni 4, mwaka huu na kufikia maamuzi hayo ya kuwafuta kazi watendaji hao wa benchi la ufundi.


"Ni kweli nimepewa barua ya kuvunjiwa mikataba yetu na kufutwa kazi pamoja na msaidizi wangu na meneja wa timu, hivi sasa najiandaa siku yoyote kuanzia leo narudi nyumbani Burundi," alisema Vivier Bahati.

Nipashe lilimtafuta Mwenyekiti wa timu hiyo, Selemani Mataso, lakini alikwepa kujibu na kudai kwamba hana hizo taarifa kwa sababu yuko jijini Dar es Salaam kwa majukumu mengine.

"Hizo taarifa bado sijapata kwa sababu niko Dar es Salaam, ila ninachojua kuna viongozi wenzangu walikuwa na kikao sasa sijajua kikao hicho kimeishaje hadi niulize," alisema Mataso.

Michezo

Jumanne Juni 7, 2022
Nipashe



Messi atupia 5 Argentina 'ikiua'

UKURASA 21

## WA KOMBE LA DUNIA...



Wachezaji wa Serengeti Girls na benchi lao la ufundi wakitinga bungeni jana, baada ya juzi kufuzu fainali za Kombe la Dunia kwa kuifunga Cameroon bao 1-0 katika mechi ya marudiano iliyopigwa Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, hivyo kuitoa kwa jumla ya mabao 5-1. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Simba, Yanga zadaiwa bil. 10/-

## ●●● Wabunge waomba zisamehewa, walia pia viwanja vya CCM huku wakitaka Ligi Kuu...

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuangalia uwezekano wa kusamehe madeni ya Sh. bilioni 10 kwa Klabu za Simba na Yanga, ambayo ni malimbikizo ya ushuru wa huduma na kodi nyingine za nyuma kabla kuanza kujiendesha katika mfumo rasmi.

**Aidha, wameitaka itunze historia ya uwanja wa TIP uliopo Kata za Manzese na Sinza, wenye historia ya kuanzishwa kwa Klabu ya Simba na Yanga miaka ya 1920.**

Mbunge wa Jimbo la Mlalo, Rashid Shangazi, aliiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kuzisamehe klabu hizo malimbikizo ya kodi Sh. bilioni 10 ya miaka ya nyuma kabla ya kuanza kujiendesha kwa mfumo rasmi.

Wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2022/23 jana, walisema kodi hizo ni kabla ya klabu hizo hazijaingia katika mfumo rasmi ikiwa ni 'service levy' (ushuru wa huduma) na kodi nyingine za serikali.

"Naiomba serikali izisamehe klabu hizi kodi hii ya miaka ya nyuma, ili ziendelee na mfumo rasmi, kuacha hivi ipo siku TRA itawafungia hatutakuwa na Yanga wala Simba, lazima hili liangaliwe,"alisema.

Naye, Mbunge wa Jimbo la Ubunge, Prof. Kitila Mkumbo, aliitaka serikali kuukarabati Uwanja wa TIP, uliopo mpakani mwa mtaa wa Chakula Bora Manzese na Sinza E, Kata ya Sinza kwa kuwa umuhimu wake ni wa kihistoria.

"Mwaka 1920 hadi 1926 ilikuwa inatwa Young Boys, walikuwa wanachezea Uwanja wa TIP na baada ya kwenda Kariakoo wakajiita Young Africans, na mwaka 1936 baada ya mambo kuwa mabaya wanashindwa sana wale jamaa wakajitoa, wakaondolewa wakaenda kuanzisha Simba, kimsingi Simba ilitokana na Yanga, waasi baada ya kufukuzwa wakabaki Yanga kupigania Uhuru,"alisema na kuongeza:

"Ule Uwanja wa TIP ni muhimu na unahitajika sana, naomba serikali iangalie kwa historia hiyo uwanja huo haupaswi kutelekezwa,"alisema Prof. Mkumbo.

Mbunge wa Jimbo la Makete, Festo Sanga, alisema bajeti imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ukarabati, na kwamba Ligi Kuu haihitaji ukarabati wa viwanja pekee, bali kuweka nyasi bandia huku akiitaka CCM kuviangalia viwanja vyake.

"Chama changu (CCM), chonde chonde tuviangalie viwanja hivi,"alisema Sanga.

Kwa upande wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, iliitaka serikali kuweka mikakati ya kuvutia wawekezaji kwenye ligi, ili kuendelea kuifanya kuwa bora zaidi katika Bara la Afrika.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stasnlaus Nyongo, akiwasilisha maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema kwa kuwa serikali imeondoa kodi za nyasi bandia kwa ajili ya viwanja nchini, iangalie namna ya kuondoa kodi katika vifaa vinavyoendana na uwekaji wa nyasi hizo katika viwanja.

## Shime: Haikuwa rahisi kufuzu Kombe la Dunia

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, Serengeti Girls, Bakari Shime, amesema haikuwa rahisi hata kidogo kufuzu Kombe la Dunia kutokana na kucheza na nchi kubwa kisoka kama Cameroon, hivyo kuwataka Watanzania wote kujivunia.

Akizungumza mjini Zanzibar baada ya timu hiyo kufuzu juzi, Shime alisema pamoja na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Cameroon, lakini kwenye mechi hiyo walicheza zaidi kwa kuulinda ushindi walioupata Yaunde ambako walishinda mabao 4-1.

Serengeti Girls imefanikiwa kutinga fainali za michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika nchini India baadaye mwaka huu, baada ya kuifunga timu ya Taifa ya Cameroon kwa bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, likiwekwa wavuni na Neema Paul dakika ya 50.

Ni matokeo yanayoivusha Serengeti Girls kwani ilipata ushindi wa mabao 4-1 ikiwa ugenini Jijini Yaounde, Cameroon Mei 22, hivyo sasa kuvuka kwa jumla ya mabao 5-1.

"Siyo hongera ya kwangu au ya wachezaji, ni hongera ya wote na ya Watanzania kwa ujumla. Nchi imekwenda kwenye Kombe la Dunia, hajaenda Shime, kila Mtanzania ana wajibu wa kufurahia, inawezekana sisi tumefanya kazi uwanjani, lakini kuna wengine walifanya twende Kombe la Dunia wakiwa nje ya uwanja, hatimaye lengo letu moja limefanikiwa," alisema kocha huyo ambaye huzifundisha timu za taifa za wanawake.

"Haikuwa rahisi, hivi ugumu ambao umeonekana leo ndiyo hivyo hivyo ulikuwa kule Yaounde, lakini leo kazi kubwa tuliyoifanya ni kuzuia ushindi wetu tulioupata ugenini, ndiyo lengo letu namba moja ingawa tumepata ushindi," alisema.

Fainali hizo zitafanyika nchini India kuanzia Oktoba 11 hadi 30, ikizishirikisha timu 16 kutoka mabara sita duniani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >